

## UTANGULIZI

Ufugaji wa kuku ni njia rahisi ya kujipatia kipato na lishe bora kwa kaya nyingi nchini, nahii imetokana na sababu kadhaa zinazo wavutia wakulima wengi kujiingiza kwenye mradi huu kama vile:

- Ufugaji wa kuku hauhitaji mtaji mkubwa kuazisha kulinganisha na mifugo mingine.
- Urahisi wa upatikanaji wa malighafi za kutumia wakati wa kuzalisha hasa vijijini.
- Mradi huchukua muda mfupi kuanza kujiendesha na kuleta faida
- Uhitaji mkubwa wa bidhaa zitokanazo na kuku kama mayai, nyama na mbolea kwaajili ya kilimo. □ Urahiisi wa kusimamia mradi.

Pamoja na kuwepo kwa fursa ya kufuga kuku, zipo changamoto kadha wa kadha ambazo wakulima wamekua wakizipata kabla na baada ya kuanzisha mradi. Hii huvunja moyo wafugaji na kukatisha tamaa hasa kutokana na upotevu wa mitaji inayowekezwa. Changamoto ambazo huwapata wafugaji ni kama zifuatazo, Gharama kubwa za chakula, Changamoto ya masoko, Magonjwa ,Upatikanaji wa aina bora za kuku, Elimu duni ya ufugaji sahihi ikiwemo; Kufuga kwa mazoea, Ujenzi wa banda bora, Malezi ya vifaranga, Utengenezaji wa chakula, Uoteshaji wa chakula mbadala, Namna sahihi ya chanjo.

Madhumuni ya kitabu hiki ni kumpa mfugaji, wanafunzi na wataalamu wengine mwongozo wa namna sahihi ya kuzitambua changamoto zinazo jitokeza na kuzipatia suluhisho kwa wakati. Na hatimae elimu ya ufugaji kitaalamu na wenye tija itaikomboa jamii kwa kuongeza uzalishaji na tija kutokana na mradi wa kuku.

## **DIBAJI**

Ufugaji wa kuku ni jambo ambalo jamii ya watanzania kwenye kaya nyingi nchini limekua likifanyika, lakini likibabiliwa na chanagamoto nyingi kwani wafugaji wengi wamekua wakifuga katika hali ya mazoea hivyo kupelekea mwendelezo wa umaskini kizazi mpaka kizazi.

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa lugha rahisi na yakitaalamu ili kubadilisha mtazamo, pia kuhamasisha wafugaji wadogo kufanya ufugaji wenye tija ulio lenga maendeleo ya kaya husika na hatimae kuinua maendeleo ya nchi kupitia kuongezeka kwa uzalishaji wa kuku na mayai. Iwapo kitabu hiki cha mwongozo kitatumika ipasavyo uzalishaji wa bidhaa bora za kuku utaongezeka hivyo kipato cha kaya kitakua na maendeleo dhahiri yataonekana. Inakadiriwa kwamba Tanzania ina kuku zaidi ya milioni 58 ambayo huchangia asilimia 30% ya pato la taifa.

Ushahidi unaonesha changamoto kubwa inayo wakabili wafugaji wa kuku ni Mgonjwa ya kuku, gharama kubwa za chakula, changamoto ya masoko, wataalamu kuwa wachache, Usugu wa kuku dhidi ya madawa, Upatikanaji wa mbinu mbadala za uoteshaji wa vyakula , ujuzi hafifu wa malezi ya vifaranga , ujenzi wa mabanda yasiyo kidhi viwango vya kufugia kuku, uvamizi wa wadudu na wezi. Kitabu hiki kimekuja na njia rahisi na maelezo ambayo mfugaji akitumia ataweza kupunguza changamoto hizo kwa kiwango kikubwa hivyo watafanya ufugaji wenye tija.

Kitabu hiki kimeandaliwa katika namna ambayo msomaji, hata kama hjawahi kufuga kuku ataweza kutekeleza yaliyo andikwa na kuelezwa bila kuhitaji usimamizi wa mtu mwingine, na iwapo yaliyoelezwa humu yatatekelezwa wafugaji watapunguza ukali wa umasikini na kuchangia kukua kwa pato la taifa kiujumla.

Mwongozo huu unaelezea changamoto na utatuzi, uzalishaji mayai na utotoleshaji, utotoleshaji na uleaji wa vifaranga, utengenezaji wa maanda, matibabu ya magonjwa, utengenezaji wa chakula, na uotesaji wa chakula mbadala. Ni adhama yangu kwamba kitabu hiki kitakua msaada mkubwa sana kwa wafugaji wa kuku na wataalamu wa kuku

## **Mada ya 1: Aina za kuku**

Kuku ni viumbe jamii ya ndege ambao wanasifa zote za kuzalisha mayai pia kufaa kwa ajiliya nyama, Kuku kipekee ni mradi ambao hauhitaji kiwango kikubwa cha uwekezaji wa fedha kwani huduma zake si ghali sana kulinganisha na aina nyingine za mifugo kama mbuzi ,nguruwe na ng'ombe

Ufugaji wa kuku hauchukui muda mrefu kuanza kupata faida mfano kuku wa nyama huweza kutumia siku 42 na 90 kwa chotara kama Sasso na Kuloirer pia kwa kuku wa mayai huhitaji muda wa miezi 5 tu kuanza kupata zao la mayai

Kuku hawahitaji chakula kiasi kikubwa sana kulinganisha na mifugo mingine hivyo gharama za ufugaji angalau zipo chini kidogo

Kuku pia hupata soko kote duniani kwa urahisi kwani walaji wa kuku ni wengi na hata dini ni chache sana zinazo kataa ulaji wa kuku

Kwahiyo ndugu nikukaribishe sana katika idara hii ya ufugaji kuku kwa ni utapata mafunzo yaufugaji pia utapata faida kwa kuuza kuku na mayai ndani ya muda mfupi.

Kuku wamegawanyika katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:

- Kuku wa nyama
- Kuku wa kienyeji/asili
- Kuku chotara
- Kuku wa mayai

### **1. Kuku wa nyama**

Hawa ni kuku ambao wanavinasaba ambavyo hupelekea kujaza nyama kwenye misuli na wanaweza kukuzwa na kuwa tayali kwa kuliwa ndani ya muda wa siku 30-42.



## **Kuku wa nyama/ Broilers**

### **1. A.Mwongozo wa ufugaji kwa kuku broiler kuku wa nyama 100**

- 1: Banda lenye madirisha makubwa weka maranda ya mbao au mpunga kutokana na upatikanaji
- 2: Weka vyanzo vya joto/ Mkaa/gesi au Umeme.
- 3: Andaa sehemu yakulelea vifaranga/brooder
- 4: Vifaa vya majina chakula,,drinkers na feeders
- 5: Hakikisha chakula na maji vinapatikana kwa wakati wote, Pia kuku walishwe kulingana nauhitaji wao ila kwa wiki tatu za kwanza walishwe masaa 24.
- 6: Kuku 100 wanahitajimfuko mmoja wa starter mifuko miwili ya grower na mfuko mmoja wa finisher.
- 7: Kuku anatakiwa kupewa chanjo zifuatazo

Sikuya 7 chanjo ya Newcastle/Kideli

Sikuya 14 chanjo ya Gumboro/IBD

Sikuya 21 rudia chanjo ya Newcastle/Kideli

8: Kuku wa nyama wanatakiwa kupewa vitamins kwaajili ya kuongeza hamu ya kula kwa siku zote watakazo fugwa, pia broilers huuzwa wakifikisha siku 28-35

**1. B. Makadirio ya bajeti ya ufugaji wa kuku wa nyama/broiler** kwa kuku 100 wa nyama/broilers kwa siku 28-30 hii inaweza kubadilika kutokana na mabadiliko ya gharama za vifaranga na malighafi nyingine

- Vifaranga 100 kwa 220000 Tsh
- Chakula Broiler starter Crumble mfuko mmoja wa 50kg kwa 69000 Tsh kila mmoja
- Broiler Grower pelets mifuko miwili ya 50kg kwa 67000 Tsh kila mmoja
- Finisher mifuko miwili kwa 66000 Tsh kila mmoja

## **Chanjo**

Newcastle siku ya saba tsh 6500

Gumboro siku ya 14 tsh 7000

Newcastle sikuya 21 tsh 6500

Neoxychick multivitamins 6000 kwa sikuya 1-5

Maranda ya mbao au ya mpunga mifuko mi nne 7000

Chanzo cha joto kwa vifaranga 30000

Hizo nigarama za lazima kwa ufugaji wa broilers

Gharamaza uendeshaji huweza kutofautiana kutoka sehemu moja na nyingine pia muda wa kulisha kuku wa nyama hutofautiana kutokana na soko namazoea ya wafugaji wenyewe, pia vifaranga hubadilika mara kwa wakati ambapo unaweza kutokea ugonjwa bandani mfugaji atatakiwa kununua dawa kama

Amplorium 10000, Tyloxoid 13000, Agracox 8000

Hayo ni makadirio kwa vitu vya muhimu kwenye ufugaji wa kuku wa nyama /broiler 100

Cha kuzingatia hapa utunze mazingira ya kuku wako ili wasiugue upunguze gharama za madawa hiyo itapelekea gharama za uendeshaji mradi kupungua hivyo faida itakua kubwa.

## **2. Kuku wa asili/ kienyeji.**

Ufugaji wa kuku wa asili ni nyenzo muhimu katika kupambana na wimbi la umasikini kwa kuongeza kipato cha kaya. Hata hivyo, pamoja na soko la uhakika, bado ufugaji kuku haujaweza kutumika ipasavyo kupambana na umaskini unao wakabili watanzania wengi na watu wenye kipato cha chini

Ni mazoea kwa jamii nyingi hapa Tanzania kufuga kuku wa asili kama sehemu ya mila na desturi zao. Kuku wa asili amekuwa akifugwa bila ya kupatiwa huduma muhimu kama makaazi bora, chakula cha ziada, tiba, kinga za magonjwa mbalimbali. Muhtasari huu unatoa mwongozo wa ufugaji wa kuku wa asili ili uweze kuzalisha na hatimae kukuza kuku kwa wingi na kupata faida



Kuku wa asili bandani

### **2.1.Sifa za kuku wa Asili**

- Wanastahimili magonjwa baada ya kupewa chanjo
- Wanaweza kujitafutia chakula
- Wanajitahidi kukabiliana na viumbe hatari
- Wanaatamia na kutotoa vifaranga pia kuwalea
- Wanazalisha mayai bora ambayo yana soko kubwa kwa walaji.

### **2.2. Usafi wa vyombo na mazingira ya kuku wa asili**

1. Uchafu ni mama wa magonjwa, hivyo zingatia haya;
2. Vyombo vya chakula na maji visafishwe mara kwa mara kwa maji safi na sabuni
3. Pumba au chakula kili cholowana na kuchanganyika na kinyesi cha kuku kitolowe na kufukiwa.



4. Choma moto au zika kwenye shimo refu kuku waliokufa kwa ugonjwa.

### **2.3. Utotoleshaji wa vifaranga**

Chagua jogoo bora natetea bora kuzalisha kuku.

#### **Sifa za jogoo bora**

1. Awe na umbo kubwa, awe na ukiko/upanga mzuri na usio angukia upande mmoja.
2. Apende kuwa na himaya yake.

Jogoo mmoja mwenye sifa hizi muweke yeye na matetea nanekumi.



#### **Sifa za tetea bora**

Tetea bora ni yule mwenye umbo kubwa, mwenye uwezo wa kutaga mayai ya kutosha, kuatamia na hatimaye kutotoa vifaranga.



#### **2.4. Uhifadhi wa mayai**

- Weka mayai mahali safi na penye hewa ya kutosha ya ubaridi.
- Tumia kasha lililokatwana kujaza mchanga/maranda safi au kasha la kuhifadhia mayai.
- Weka sehemu butu ya yai iwe upande wa juu na ile iliyo chongoka itazame chini.
- Andika namba au tarehe katika siku lilipotagwa.
- Mayai yakisha tagwa yatolewe na kuhifadhiwa na moja liachwe kwenye kiota ili kumuita kuku kuja kutaga kesho yake.

#### **2.5. Makala juu ya mayai ya kuku na utotoleshaji**

Mayai ya kuku huanguliwa kwa siku 21 kabla ya vifaranga kutotolewa

Uatamiaji wa asili na utotoleshaji vifaranga:

Mayai kwa ajili ya kuatamiwa ni lazima yawe mapya;

Umri wa mayai baada ya kutagwa usiwe zaidi ya siku kumi (10) na yawe yamehifadhiwa katika sehemu yenye ubaridi usiozidi nyuzi joto 20°C .Iwapo hali ya joto iko juu kuliko 20°C basi mayai ya kutotoa vifaranga yasihifadhiwe kwa zaidi ya siku tano (5).

Ili kupata matokeo mazuri, mayai ya kuatamiwa (mayai yaliyo chaguliwa) yanatakiwa yawe na umbo la kawaida na ukubwa wa wastani kwa aina ya kuku wanaohusika.

Ganda la mayai ya kuangua lisiwe na mikwaruzo au nyufa kwani likiwa na nyufa yai hupoteza unyevunyevu ambao ukipungua kiiini cha yai kinaweza kufa au linaweza kuingiza vimelea kama fangasi na bakteria ambavyo husababisha kutotolewa kwa vifaranga wenye afya mbaya au walikufa.

Hifadhi mayai ya kuangua kwenye makasha makavu ndani ya shimo lililopo ardhini katika sehemu yenye ubaridi kuliko sehemu zote ndani ya chumba.



### **Mayai yamehifadhiwa**

Kabla mayai hayajaatamiwa chunguza mayai ambayo yana mbegu na yale yasiyo na mbegu . Mayai ya kuku aliyepandwa na jogoo

yanakuwa na mtandao wa mishipa ya damu mapema sana ambayo inaweza kuonekana kwa kutumia mwanga mkali wa kurunzi.


Baada ya mayai kuatamiwa kwa siku saba hadi kumi yanaweza kuchunguzwa mayai yasiyorutubushwa na yenye viini vilivyokufa yanaweza kutambuliwa katika siku saba baada ya kuanza kuanguliwa

Wakati wa kupima kwa kutumia mwanga wa kurunzi mayai yaliyo rutubishwa yanakuwa na mishipa ya damu inayo onekana, na doa jeusi ambalo ndicho kiini cha uhai.

Iwapo kiini cha uhai kimekufa, kina onekana kama kitu cha mvingo mfano wa pete kuzunguka kiini hai.

Mayai ambayo hayaja rutubishwa yanakuwa na nafasi kubwa ya hewa na kiini cha uhai kinao nekana kama kitu cheusi ndani ya ndani ya yai.

Mayai ambayo hayaja rutubishwana na yale yenye viini vilivyo rutubishwa inabidi yatengwe na kuondolewa ili yasije yakaozea ndani ya kiota, yakapasuka na kuharibu mayai mazuri ambayo yapo katika kuatamiwa.



**Yai lililorutubishwa**



**Yai lisilo rutubishwa**

## **2.5. Kutotolesha vifaranga wengi kwa wakati mmoja**

- Kama unataka kuku zaidi ya mmoja waatamie na kutotoa kwa wakati mmoja fanya ya fuatayo
- Kuku wa kwanza akianza kuatamia muwekee mayai yasiyo na mbegu mfano mayai ya kuku wa kisasa au kuku asiye na jogoo.
- Rudia zoezi hilo hadi utakapo fikisha kuku watano kisha wawekee kuku wote mayai yenye mbegu

## 2.6. Kuku anae atamia mayai

Kuku anaye atamia atengwe katika kundi ili asisumbuliwe na kuku wengine ,

Mtengee kuku kiota ambacho kinampa nafasi ya kupata maji safi na chakula kwa karibu.

Kiota au kikapu ni lazima kiwe kikubwa kiasi cha kumpa kuku nafasi ya kuatamia mayai yote.



Weka matandazo makavu ambayo ni mapya yaliyo nyunyizwa majivu kidogo kuzuia visumbufu kama utitiri

Wapo vifaranga wanao totolewa ni wachache njia nzuri ya kuatamia mayai ni kumtumia kuku kuliko mashine ya kutotolesha vifaranga kwasababu kuku ana uwezo mkubwa wa kutotoa vifaranga kwaasilimia 80- 100 ukilinganisha na mashine ambayo hutotoa mayai kwa asilimia 60-85 kama itakua kwa kiwango kizuri.

Vifarangawakishatotolewawannawezakulelewa kwa kumtumia mama ikiwa ni wachache. Lakini vifaranga wanaweza kulelewa kwa kutumia kifaa maalumu cha kulelea brooder.

### **Kutotolesha kwa njia ya mashine/Incubator**

Incubator ni kifaa maalumu ambacho hutumika kutotolesha vifaranga badala ya kuatamisha kwa kuku mwenyewe, mayai huwekwa kweye mashine hii kwa muda wa siku 21 kama inavyo fanyika kwa kuku. Ifikapo siku ya 18 baadhi ya mayai huanza kuanguliwa na mpaka siku ya 21 mayai yote yenye vifaranga huwa yamekamilika kuanguliwa inabidi vifaranga watolewe na mayai yaliyo haribika yafukiwe au kutupwa mbali na eneo ambapo umeweka mashine yako.

### **Mambo ya kuzingatia kwenye matumizi ya mashine ya kuangulia mayai**

- Hakikisha mayai yamerutubishwa na jogoo
- Mayai yasikae zaidi ya siku nane baada ya kutagwa kabla ya kuwekwa kwenye mashine
- Hakikisha umeme unakuwepo muda wote ili kuzuia mayai kupoa kwa kupungua joto kwenye mashine, nunua jenereta kwa matumizi ya dharula
- Joto la kuatamishia mayai kwenye mashine liwe kati ya 37-39°C kwa siku 18 za kwanza na kasha lipunguzwe mpaka 36.5°C kwa siku tatu za mwisho
- Unyevu kwenye mashine unatakiwa kuwa kati ya 60-65, wakati wa kukaribia kuangua vifaranga pandisha mpaka 70
- Hakikisha mzunguko wa hewa ni mzuri kufanya Oxygen ipatikane bila kuathiri joto na unyevu

- Mji kwaajili ya unyevu ya kiisha au kupata joto ya badilishwe.
- Zingatia usafi kwenye chumba cha kutotoleshea vifaranga, safisha kwa maji yenye dawa.



## **Mashine za kutotoleshea vifaranga**

### **3. Kuku chotara**

Hawa ni kuku ambao wamepatikana kwa kufanya cross kati ya kuku wa asili/ kienyeji na majogoo bora kwaajili ya nyama na mayai. Kuku hawa wanao uwezo wa kufugwa kwenya mazingira ya kawaida kama ilivyo kwa kuku wa kienyeji

Kuku chotara wanaweza kufugwa katika aina zote za ufugaji ikiwepo, Ufugaji wa ndani, Nusu huria na Huria muda wote kujitafutia chakula

#### **3.1. Sasso**

Ni kuku chotara ambae amepatikana kwa kufanya cross kati ya kuku wa kienyeji/kuku wa asili na jogoo bora wa nyama, Sasso anaweza kufugwa kwaajili ya kuzalisha nyama na mayai.

Akifugwa kwa ajili ya nyama na kupewa chakula cha kunenepesha wanaweza kufikisha zaidi ya kilo mbili na nusu ndani ya muda wa siku 70-90 (miezi mitatu).

Wakifugwa kwa ajili ya mayai wanaanza kutaga wakiwa na umri wa wiki 20 (miezi mitano) ambapo kwa muda wote tangu kuanza kutaga wana uwezo wa kutaga mpaka mayai 240



**Sasso wakiwa bandani**



### **3.2.Mwongozo wa ufugaji Sasso/Kuroiler/ Tanbro kwa ajili ya nyama**

Sasso anatakiwa kupewa chakula kwa mtiririko ufuatao

Broiler Starter Crumble siku 1-18 (akifika uzito wa gramu 400 unaweza ukaanza kumpa grower)

Broiler grower pellets siku 19-35

Broiler finisher pellets 36 mpaka siku ya kuuza

### **3.3.Sasso/Kuroiler akifugwa kwaajili ya mayai**

Apewe chakula kwa ratiba ifuatayo

Broiler starter Crumble siku 0-13 (usishtuke ndo mwongozo sahihi mpe starter ile ya broiler)

Layer starter mash siku 14-41(wiki 3-7)

Layer grower mash siku 42-111(wiki 8-18) au mpaka kuona yai bandani

Complete layer mash siku 112(Wiki 19) baada ya kuona yai bandani hadi kuuzwa.

Zingatia kuku hutakiwa kulishwa kwa kufuata kiwango cha chakula kutokana na umri kama ilivyo kwa kuku aina nyingine

Zingatia Sasso/Kuroiler anahitaji kukaa mahala pasafi, penye mzunguko mzuri wa hewa na hataki stress za mara kwa mara

### **3.4.Kuroiler**

Hawa ni kuku chotara ambao wamepatikana baada ya kumpandisha kuku tetea wa asili na Jogoo bora la kuku wa mayai na asili yao ni India, Kuloirer hufugwa kwa ajili ya nyama na mayai.

Kuku hawa wakifugwa kwaajili ya mayai hutaka mayai 240-300 kwa muda wa miaka miwili na nusu, kuku hawa wanaweza

kufugwa kwa mifumo yote mitatu , Kufugiwa ndani, Kufugwa nusu huria na Huria

### **3.5. Sifa za kuroiler**

Unaweza kuwafuga katika mazingira ya kawaida

Unaweza kuwafuga kama Kuku wa kienyeji au Ukawafuga kisasa kwa kuwaweka ndani ya banda ila wawe huru, Inamaana hata gharama za kuwahudumia ziko chini sana ukilinganisha na kuku wengine.

Kuku hawa ni wastahimilivu wa Magonjwa, hivyo uwezekano wa kupata hasara kupitia magonjwa ni mdogo (kama utawapatia chanjo kwa wakati na chakula kizuri na kufuata kanuni bora za ufugaji kuku)

Kuroiler huanza kutaga wakiwa na Miezi 5 Tu (Tofauti na kuku wa kienyeji wa hapa nchini ambao huanza kutaga wakiwa na Miezi 6)

Kuroiler hutaga kwa Muda wa Miaka Miwili. (Yani utauza mayai Mpaka uchoke wewe) ukizingatia ulishaji sahihi

Kuroiler ni wazuri kwa Nyama pia kwa maana Majogoo hufikisha uzito wa hadi Kilo 5 na Mitetea hufikisha kilo 3.5 hadi 4.

Mayai yao ni fertile (yani yana mbegu na yanaweza kutotoleshwa) Ila hawalalii, Inamaana ukitaka kutotolesha inabidi uatamize kwa kuku wengine wa kienyeji , Au utumie Incubators ambazo tunazo pia na unaweza kuzipata kwa gharama nafuu.

Soko la kuku hawa kubwa mno kwa maana ni wazuri kwa mayai na nyama. (Nb: Ni muhimu kufanya utafiti wa Soko lako kabla ya kuanza kufuga, kwasababu maeneo yanato fautiana)



### **Kuroiler wakiwa bandani**

#### **4. Kuku wa mayai**

Hawa ni kuku ambao wamezalishwa kwa jogoo bora wa mayai na tetea anaetaga mayai mengi kwa mwaka, kuku hawa pia wana

vinasaba ambavyo uwafanya kutaga mayai mengi wa msimu wa utagaji ukilinganisha na kuku wengine kama chotara na kuku wa asili. Kuku hawa wanao uwezo wa kutaga mayai 300-340 kwa kipindi cha wiki 81 ambazo watafugwa.

Zipo aina tofauti za kuku wa mayai kama vile;

- Isa brown,
- Rhode Island,
- Hy-line,
- Bovan Brown,
- Lohman n.k

Kuku wa mayai wanaweza kufugwa kwa namna mbili ambazo ni nusu huria na mfumo wa kuwaweka bandani muda wote, kama ilivyo kwa kuku wengine hawa nao pia wanahitaji banda bora na kupewa chakula chenye mchanganyiko mzuri na sahihi kuwezesha utagaji kuwa wa kiwango cha juu.

Ulishaji wa kuku wa mayai unatakiwa kuzingatia kiwango sahihi cha chakula kama ilivyo ainishwa kwenye ratiba ya ulishaji hapa chini, pia inashauriwa kuku hawa kupewa chakula mara mbili kwa siku ikiwa 40% ya chakula anachopewa kwa siku kitolewe asubuhi na 60% wapewe jioni.

### **Kuku kwenye sakafu/ Floor system Faida**

- Kuku huendeleza tabia zao za asili kama kuparua
- Ni rahisi kujua maendeleo ya kuku na mabadiliko

yanayo wapata kuku Hasara

- Mayai huchafuka na kupasuka
- Kuku kudonoana
- Magonjwa hujitokeza kama usafi haujazingatiwa
- Chakula ma maji humwagika



### **Kufuga kuku kwa njia ya cages**

Cages ni njia ya kisasa ya kufuga kuku wa mayai, inayo wezesha kufuga kuku wengi katika eneo dogo. Unatakiwa kujenga banda lenye kuruhusu hewa kuingia na kutoka kasha ndani yake utaweka cages za kufugia kuku. Kuku wanatakiwa kuhamishiwa kwenye cages wafikapo umri wa wiki 13-15 hii huwa wezesha kuzoea mazingira mapya kipindi watakapo anza kutaga hawatakua na msongo,

### **Faida za cages**

- Hurahisisha ukusanyaji wa mayai
- Mayai hayapasuki na kuchafuka
- Kuku hawali mayai na kudonoana hupungua
- Magonjwa hupungua kwa kiasi kikubwa
- Nirahisi kufanya usafi
- Kuku wengi wanafugwa katika eneo dogo
- Nirahisi kulisha na kuwapa maji
- Asilimia ndogo ya chakula ma maji hupotea



## **Kuku wakiwa kwenye cage**

### **4.1.Ulishaji wa kuku wa mayai (layers)**

Kuku wa mayai ili watage vizuri wanatakiwa walishwe chakula bora kwa utaratibu unaotakiwa, ukiwazidishia au kuwaongezea hawatotaga vizuri kwa kuwa watanenepa na kujaza kiwango kikubwa cha mafuta kupita kiasi.

Wanatakiwa walishwe kati na kati kulingana na umri kama ifuatavyo

Umri wa wiki 1 -2

Katika umri huu wanapewa chakula aina ya "Super Starter" kwa ajili ya kuwatengenezea kinga mbadala ili waweze kuhimili mikiki mikiki ya vijidudu vya magonjwa kadri wanavyoendelea kukua, wanapewa chakula hicho kwa kiwango maalum kama ifuatavyo:-

Wiki ya 1: Gramu 12 kwa kuku mmoja kwa siku moja Wiki

ya 2: Gramu 22 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Umri wa wiki 3 - 8

Hapa wanakuwa bado ni vifaranga na wanapewa chakula aina ya "Chick Starter" kwa ajili ya kuendelea kuwajenga miili yao waweze kupoekea virutubisho vizuri, hii inatokana na kwamba kuna baadhi ya viinilishe vinafanya kazi ya kumeng'anya chakula na kupatikana viinilishe vingine, kwahiyo vikikosekana katika mwili wa kuku basi hata wale chakula gani bora, hawawezi kutoa mazao bora, lakini kwa kuwapa "Chick Starter" itawapelekea kuwa na virutubisho hivyo muhimu.

Kiwango na ulishaji wake ni kama ifuatavyo:-

Wiki ya 3: Gram 27 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 4: Gram 32 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 5: Gram 38 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 6: Gram 42 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 7: Gram 46 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 8: Gram 50 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Umri wa wiki 9 - 18

Katika umri huu kuku wanapewa chakula aina ya "Grower Mash" kwa ajili ya kuwakuza na kuwajenga mfumo wa uzazi kwa maandalizi ya utagaji. Kiwango cha chakula kinategemea na wiki kama ifuatavyo:-

Wiki ya 9: Gram 56 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 10: Gram 62 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 11: Gram 64 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 12: Gram 66 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 13: Gram 68 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 14: Gram 74 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 15: Gram 74 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 16: Gram 80 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 17: Gram 82 kwa kuku mmoja kwa siku moja Wiki

ya 18: Gram 88 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Umri wa wiki 19 - 40

Huu ni umri ambao kuku wanataga kwa kiwango kikubwa sana (85% hadi 100%) hali ambayo inawafanya kutumia nguvu nyingi mno, hivyo hupewa chakula aina ya "Layers Phase 1" kwa ajili ya kufidia nguvu ya ziada wanayotumia ili waendeleo kutaga kwa kiwango hichohicho. Ulishaji wake ni kama ifuatavyo:- Wiki ya 19: Gram 92 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 20: Gram 102 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 21: Gram 108 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 22: Gram 114 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 23: Gram 116 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 24: Gram 120 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Wiki ya 25 - 40: Gram 130 kwa kuku mmoja kwa siku moja

Umri wa wiki 41 - 80



Katika umri huu kuku wanakuwa wameanza kuchoka na huanza kutaga kwa kiwango cha kawaida (65% hadi 75%) hivyo hupewa chakula aina ya "Layers Phase 2" kwa ajili kuendeleza (maintain) kiwango chao hicho kwa muda mrefu. Kiwango chao ni "Gram 130 kwa kuku mmoja kwa siku moja".

NB: Kuanzia wiki 81 na kuendelea unaweza kuwauza na kuweka kuku wengine kwa sababu kiwango cha utagaji hupungua na utapata hasara ya chakula, vilevile idadi ya vifo huongezeka.

## **Mada ya 2: Maandalizi ya banda la kuku**

Kuku ni viumbe ambao wanahitaji matunzo mazuri ili waweze kuzalisha mayai au kukuavizurikwawakati

### **2.1. Yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa wakati wa maandalizi ya banda**

Banda zuri la kuku linatakiwa kuwa na nusu tofali/ukuta na nusu waya au kujengwa kwa bati/mbao kuruhusu mzunguko wa hewa bandani ukuta unatakiwa kuwa 0.5m-0.8m banda hilo lifungwe vizuia upepo au baridi (Caterns).

Banda lakuku linatakiwa kuwa mbali kidogo na makazi ya viumbe wengine kama mbwa, nguruwe, mbuzi na bata kuzuia magonjwa kwa sababu mifugo hiyo huwani wahifadhi wa baadhi ya vimelea vya magonjwa. Wakati kwa mabanda yanayo tazamana/ ambayo yapo paralle inabidi iwekuanzia mita 100 kutoka banda moja hadi jingine na mabanda yanayo fuatana yanaweza kutofautishwa kwa mita 20.

Banda lizingatie uelekeo wa jua yanani litazame uelekeo wa Mashariki kwenda Magharibi, pia Lizingatie uelekeo wa upepo kuruhusu hewa chafu kuondolewa bandani

Banda la kuku linatakiwa kuwa na sakafu nzuri ambayo itakua rahisi kusafisha kuzuia vimelea vya magonjwa. Inaweza kujengwa kwa kuchanganya cement na nzege/concrete au udongo wa kichuguu utakao sakafiwa kurahisisha usafi.

Banda la kuku linatakiwa kuezekwa hasa kwa bati kurahisisha usafishaji japo unaweza ukaezeka kwa kutumia aina yoyote ya vifaa vya kuezekea isiyo pitisha mwanga wa jua na mvua.

Banda la kuku linatakiwa kusafishwa na kuachwa wiki mbili hadi nne bila kuku baada ya kutoa kuku ilikuingiza kuku wengine hii inasaidia kuua mzunguko wa ukuaji wa vimelea vya magonjwa. tumia dawa za kuua wadudu kama TH4 au V-RID

Siku moja kabla ya kuingiza kuku hakikisha maranda yameingizwa bandani kwa ujazo wa kina/diameter ya 5cm kuruhusu joto kuwepo pia ilivumbi la maranda lipungue kuruhusu hewa isiyo navumbi wakati wa kuingiza vifaranga.

Vifaa vyote vitakavyo tumika kipindi cha kufuga kuku kama drinkers, feeders, mifuko, brooder, vyungu vya moto viwepo bandani kabla vifaranga hawajaletwa na view vimepuliziwa dawa (disinfectant kama V-RID) ila vinywesheo vya maji na vilishio vya chakula vioshwe kabla ya kutumia kwa vifaranga.

Hakikisha chanzo cha joto kinakuwepo ndani ya banda la kuku na uwashe masaa 24-48 kabla ya kuingiza vifaranga ili sakafu ipate joto hii itasaidia vifaranga kuto kutana na baridi Kali ya kwenye sakafu.

### **Mfano wa vyanzo vya joto**

- Vyungu au majiko ya mkaa
- Bulb za joto (wati 100-200)
- Taa maalumu za joto (Infrared bulbs)

- Brooder ya gesi
- Heater za umeme



### Vyungu vya joto kwa vifaranga



## **Brooder ya gesi**

Hakikisha kuna sehemu ya kunawa mikono kwa dawa/disintectant au sabuni kama Detto kabla ya kufanya chochote ndani ya banda, au kugusa vifaranga, pia sehemu ya maji yenye dawa ya kukanyaga /footbath, dawa ibadilishwe kila siku kuua vimelea vya magonjwa kutumia (farm guard) au Virocid.

Hakikisha banda la kuku linakua kavu muda wote ili kuzuia magonjwa ya Coccidiosis na yale yamfumo wa hewa hii unaweza kwa kuweka vinywesheo /Drinkers juu kidogo kulingana na ukubwa wa vifaranga au kuku wako.

NB: Hakikisha mwanga, hewa na joto vinakuwepo muda wote wa kufuga kuku kwa kuzingatia hatua ya ukuaji wa kuku.

### **2.2. Banda la kuku wa mayai**

Ujenzi wa banda sahihi huenda sambamba na aina za kuku na umri wa kuku wenyewe kwa kuku wa mayai kama Issa bown, Hy- line, Bavon brown, Rhode island , Mita moja mrabai 1nachukua kuku 78. Na kwa kuku chotara mfano Sasso, Kuloirer, Kenbro na Tanbro mita moja mraba inachukua kuku 4-5.

Mfano unataka kujenga banda la kuku wa mayai 728

Urefu  $13 \times$  Upana  $7=91m^2$

Kwahio  $91m^2 \times 8$  idadi ya kuku kwa mita moja mraba = 728 kuku wanaotakiwa kuwepo bandani.

Hili banda linatakiwa kuwa na sehemu yakutagia/Nest box, Ambapo chumba kimoja cha kutagia kinatakiwa kutumiwa na kuku 4-5 hivyo angalia idadi ya kuku na ufanye uwiano kujua utahitaji viota vingapi bandani.

Pia banda linatakiwa liwe na sehemu ya mazoezi au perches, sehemu ya kuku kuruka ruka na kulala juu.



**Banda la kuku**



**Kiota cha kutagia**

### **2.3. Banda la kuku wa nyama/broiler**

Kuku wa nyama wametengenezwa kwa lengo la kuwakuza ndani ya muda mfupi kwaajili ya kuzalisha kiwango kikubwa cha nyama na vipimo vyake vya kitaalamu ni kama ifuatavyo. Mita moja mraba kwa broiler inachukua kuku kumi.



**Banda lililojengwa kwa mbao na wavu na kuezekwa kwa bati**



## **Kiota cha kutagia**


### **Mada ya 3: Ulinzi wa viumbe hai (kuku) dhidi ya magonjwa**

Magonjwa ya kuku imekua fimbo kubwa sana kwa wafugaji hali inayo pelekea kuongezeka kwa gharama za matibabu kwa kununua dawa, pia hupelekea kuku kupungua uzito na hivyo thamani yao sokoni huwa ndogo, hupelekea vifo vingi hali inayo poteza mitaji na hatimae kukata tamaa ya kufuga.

#### **3.1.Mbinu za kupunguza magonjwa kwenye shamba la kuku**

- Usimamizi mzuri wa kuku, hasa mtunzaji awe mchunguzi kubaini maendeleo ya kuku na kutatua changamoto zinazo wakabili kwa wakati
- Banda lijengwe katika ubora unaotakiwa, ukuta wa tofali/mabanzi nusu (0.5m), na senyenge /chicken mesh 1.8m, banda liwe na uelekeo wa kutoka Masharikimagharibi na lijengwe kwa kutazama uelekeo wa upepo, sakafu ijengwe kwa cement iliyo changangwa na mchanga Rough cement, au iliyosakafiwa kwa udongo wa kichuguu

- Weka sheria za kufuata ili kuwakinga kuku wako dhidi ya magonjwa, mfano ziwepo nguo na Mabuti maalumu ya kuingilia bandani, vifaa vya kuku visihamishwe kutoka banda moja kwenda jingine, weka maji yenye dawa ya kukanyaga unapoingia na unapo toka bandani kama Farm guard kwa ajili ya kuua vimelea



### **Safisha mikono kwa sabuni**

- Usichanganye kuku na aina nyingine ya ndege kama Bata, kanga, njiwa pia banda lako liwe mbali na mifugo ya aina nyingine kama ng'ombe, mbuzi , kondoo na nguruwe.
- Kwa uwekezaji mkubwa hakikisha banda la kuku lipo mbali kidogo na makazi ya watu , pia umbali kutoka banda hadi banda usipungue 100m kwa mabanda yanayo tazamana na upishanishe mabanda kwa 20m kwa yanayo fuatana.
- Kuku apate maji na chakula kisafi kupunguza magonjwa kama Typhoid
- Banda lisafishwe kwa maji yenye dawa V-RID au TH4 na lipumzishwe angalau kwa wiki 1-2 kabla ya kuingiza kuku wengine bandani.
- Zuia uingiaji wa watu bandani, anaeingia bandani awe ni muhudumu wa kuku pekee au mtaalamu atakae kuja kuwatibu kuku wako kama wataugua. Pia magari au



vyombo vingine vikanyage maji yenye dawa au kupuliziwa maji yenye dawa kabla ya kuingia bandani

- Wape kuku wako chanjo dhidi ya magonjwa ya virusi Kama kideli, gumboro, ndui, mareks, Kwa kufuata ratiba sahihi ya chanjo.
- Epuka kuchanganya chakula kwa kutumia mazao yaliyo vunda na kuoza, kwani hupelekea magonjwa ya matumbo
- Uonapo dalili za kuku watenge kisha utafute usaidizi wa daktari au mfugaji mzoefu wa kuku akusaidie kuwa hudumia kuku wako, hakikisha unawapa kuku wako dozi mpaka iishe kwa kufuata maelezo sahihi ya matumizi ya dawa.
- Banda liwe kavu muda wote kupunguza magonjwa ya homa za matumbo kama Koksidiosis, kwa kuyageuza Maranda angalau mara mbili kwa wiki au kubadilisha Maranda marayatakapo loana.
- Vyombo vya kuwekea maji vinatakiwa kuwa visafi muda wote, maji yanayobakia kwenye vinywesheo ya mwagwe na maji safi yaongezwe.
- Joto sahihi liwepo wakati wa makuzi ya vifaranga kwa kuwatengenezea kinengu nengu/ Brooder, ambapo utawawekea chanzo cha joto kama Vyungu, Gesi, Bulb, Viga, Infrared kutokana na uwezo na upatikanaji.
- Weka utaratibu wa kunawa mikono unapoingia na unapotoka bandani kwa sabuni au dawa za kuulia wadudu kama Ethanol au spirit.
- Mizoga yote ya kuku izikwe au ichomwe mbali na eneo unalo fugia kuku, pia usimwage mbelea ya kuku karibu na Banda la kuku
- Safisha mazingira kuzunguka banda la kuku kuzuia ueneaji wa magonjwa na

Uzalianaji wa wadudu Kama nzi na mbu, fyeka nyasi na fukia vidimbwi vya maji.



**Kanyaga maji yenye dawa**

#### **Mada ya 4: Magonjwa ya kuku, dalili na tiba**

Kama viumbe wengine kuku amekuwa akisumbuliwa na magonjwa ya aina mbalimbali, hivyo ni vema kuainisha na kutambua baadhi ya dalili za magonjwa ambapo zipo dalili kuu na dalili za kawaida. Dalili kuu ni zile zinazo thibitisha kwamba kuku anaumwa ugonjwa Fulani wakati dalili zisizo kuu hujitokeza kwa magonjwa mengi hivo hazithibitishi ugonjwa halisi

##### **4.1. Visababishi vya magonjwa**

- Virusi
- Bakteria
- Protozoa
- Viroboto/utitiri
- Minyoo

##### **4.2.Magonjwa ya kuku**

## **New Castle Disease/mdondo/kideli**

Huu ni ugonjwa wa virusi ambao huwapata kuku wa aina zote na wa umri, ugonjwa huu huenea kwa haraka kwa makundi yote ya ndege, huweza kuua kuku mpaka asilimia 100% **Ueneaji wa ugonjwa**

- Watu au vifaa vya kubebea kuku huweza kueneza ugonjwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine
- Kuku kuvuta hewa yenye virusi vya ugonjwa
- Ndege walao mizoga wanaweza sambaza ugonjwa kwenda sehemu nyingine
- Kuku wazima kuchanganyana na wazima

### **Dalili kuu**

1. Kupindia shingo juu au chini au nyuma.
2. kuzunguka zungunga,
3. Kuharisha rangi ya kijani
4. Vifo mfululizo
5. kuku kutembea kwa kurudi nyuma kichwa kikiwa juu,
6. kuku kuwa kama na kifafa na kuangukia upande mmoja


**Dalili isiyo kuu** ni mharo wa rangi ya kijani

**Matibabu:** Hakuna tiba kwa kuwa ni ugonjwa wa virusi,

Kuku wapewe kinga siku ya 7, 21 na kila baada ya miezi mitatu,

Kwaajili ya kutibu hizo dalili hapo tumia dawa ya Trimazine 30% au Trimafarm + vitamins.

**NB: Usichanje kuku wakati ugonjwa umeshaingia bandani, chanjo ya ugonjwa itunzwe katika mazingira ya ubaridi.**



### **Dalili ya mwisho ya kuku mwenye kideli**

- **Gumboro / infectious bursal disease**

Huu ni ugonjwa wa virusi ambao huathiri kuku wakiwa na umri wa wiki tatu za kwanza katika hatua ya vifaranga

**Dalili luu:** Mharo rangi nyeupe kama chokaa

Wape kinga kuku wako siku ya 14 kisha rudia siku ya 28



### **Kuku mwenye gumboro anavimba bursal**

- **Marek's /mahepe**

Huu ni ugonjwa wa virusi ambao huwapata kuku wanao kaa kwa muda mrefu kama kuku wa mayai (chotara, l ayers pure hata kuku wa kienyeji). **Ueneaji**

- Huenea kupitia mfumo wa hewa kwa vumbi lenye vimelea

- Mte ya kuku wagonjwa
- Binadamu na aina nyingine za wadudu na wanyama huweza kusambaza maambukizi' **Dalili kuu:**

- kupooza/ kukakamaa kwa miguu na mbawa mguu mmoja mbele na mguu mmoja nyuma, pia kihifadhia chakula (Crop) huvimba.
- Kuku huathiriwa wakiwa wadogo ila madhara huonekana pindi wanapofikia umri wa kuanza kutaga mayai.
- Mboni ya jicho kuwa na rangi ya kijivu
- Vifo kati y 10-80%

**Hakuna tiba:** kuku wapewe chanjo ya Marek's siku ya kwanza baada ya kuanguliwa.

- **Ndui ya kuku(Fowl pox)**

Huu ni ugonjwa wa virusi, ambao huenea kwa haraka kutoka kwa kuku mmoja kwenda kwa mwingine hushambulia kuku wakubwa na wadogo, chanzo kikuu huwa ni ndege wengine kama bata

### **Uenezwaji**

Ugonjwa huenea kutoka kwa kuku mmoja kwenda kwa mwingine kupitia majeraha ya kuku mgonjwa

Mbu na wadudu wengine wanaweza kueneza kwa kumuuma kuku mgonjw kasha kumuuma kuku mzima

### **Dalili kuu:**

- Kuota kwa vipete sehemu zisizokua na manyoya kama kilemba cha kichwani (comb & wattles),puani, kuzunguka

macho,kwenye mwili maeneo ya mgongo pasipo na manyoya pia miguuni.

- Kupoteza hamu ya kula
- Vipele hupasuka na kuacha vidonda
- Homa kali
- Macho kuziba



**Kuku wanao umwa ndui**

**Hakuna tiba kwani ni ugonjwa wa virusi**

**Kinga**

- kuku apewe chanjo siku ya 30
- Watenge kuku wazima na wagonjwa
- Fukia na kuzuia mazalia ya mbu karibu na banda la kuku

Kupunguza madhara kuku aoshwe kwa maji ya vugu vugu mapaka vipele viishe na uvipake Mafuta, pia mpe Ant-biotic kama OTC 50%

- **Mafua makali/ coryza**

Huu ni ugonjwa wa virusi ambao huathiri sana mfumo wa hewa/upumuaji wa kuku **Dalili kuu:**

1. Kupiga chafya
2. Kusinzia

3. Kukoroma
4. Kuvimba macho, kichwa na ute mzito mweupe kwenye jicho
5. Mucus/mlenda puani na mdomoni ukimchunguza

## **Matibabu**

Tylodox, Fluban, Enrovet au OTC 50% changanya na vitamins. Pia hakikisha kuna mzunguko mzuri wa hewa bandani na pia Maranda bandani yasiwe na vumbi



## **Kuku anae umwa mafua makali**

- **Fowl typhoid/homa ya matumbo**

Huu ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria wanaoitwa Salmonella na huwapata kuku wa kila umri, huenea kutoka kwa kuku wazima kwenda kwa kuku wagonjwa kupitia maji, chakula na kinyesi cha kuku wagonjwa na wadudu kutoka banda jingine kuja kwenye shamba lako.

## **Dalili kuu:**

- Mharo rangi ya njano, kijani na nyeupe
- Vifo vichache kwa muda mrefu
- Manyoya kusimama

- Kinyesi kuganda sehemu ya nyuma
- Kiwango cha utagaji kushuka **Kuzuia**
- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa
- Kuku wakubwa watenganishwe na kuku wadogo
- Safisga vyombo vya chakula na maji

**Matibabu:** Esb 3, Trimazine 30%, Enrovet, Ganadexil na Limoxin kwa kuzingatia maelekezo ya dozi sahihi.

- **Coccidiosis /kuhara damu**

Huu ni ugonjwa unao athiri tumbo la kuku, ukimpasua anakua na vidonda tumboni na kwenye utumbo, ugonjwa huu husababishwa na protozoa na huathiri sana kuku wadogo.

Huambukizwa kwa kula chakula au maji yenye vimelea vya ugonjwa

**Dalili kuu:**

- Kinyesi rangi ya ugoro ugonjwa unapoanza, kisha hufuatiwa na mharo au kinyesi kilicho changanyika na damu
- Kuku kudhoofu na kushuka uzito
- Kuku kusinzia na kushusha mabawa
- Kuku kujitenga mbali na kundi

**Matibabu:** Amplorium 20%, Esb 3, Trimazine 30%, pia unaweza kuwapa Vitacox au Agracox kama kinga wakiwa vifaranga, dawa zore zenye mchanganyiko wa salpha hutibu ugonjwa huu.

- Hakikisha banda lako ni kavu muda wote kuzuia uzalianaji wa bakteria waletao ugonjwa huu.
- Zingatia usafi wa vyombo vya maji na chakula





### **Kuku anaemwa koksidiosis**

- **Fowl cholera/ kipindupindu cha kuku** Huu ni ugonjwa unao sababishwa na bakteria **Dalili za ugonjwa:**
- Kinyesi/mharo rangi ya njano
- Kuhema kwa shida
- Kulala wakati kichwa ameingiza kwenye mabawa
- Kuwa na uvimbe kwenye mikunjo ya miguu

**Matibabu:** Trimazine 30%, Trimafarm, Esb3 na Oxytetracycline (OTC)

Zingatia usafi wa wa vyobo vya chakula na maji

- **Infectious Bronchitis**

Husababishwa na virusi na huzaliana kwa muda mfupi ndani ya siku 1-4

**Dalili:** kuku hupata shida ya kupumua, kuku anapiga kelele na chafya, macho na pua hutoa maji pia wanatikisa vichwa, huambatana na kuongezeka kwa vifo bandani

Wape kuku wako kinga sambamba na Newcastle siku ya saba

## **Magonjwa yatokanayo na lishe duni**

- Dalili kuu: Kuku kuvimba macho, miguu kukosa nguvu na kushindwa kusimama, kutaga mayai yenye gamba laini, kula mayai na kudonoana

## **Matibabu**

1. Chakula kiwe na mchanganyiko mzuri wa vitamin A
2. Chakula kiwe na madini ya kutosha na protini (Calcium na phosphorus) wawekee chokaa ya kuku, DCP au mifupa
3. Kwa wanaodonoana unaweza kukata midomo yao au kuichoma midomo yao chini ya uangalizi wa daktari wa mifugo kisha uwape vitamins kwa wingi

## **Utambuzi wa magonjwa ya kuku kwa rangi ya kinyesi**

- **Mharo mweupe** (pollorum bacillary diarrhoea) ugonjwa huu huathiri zaidi vifaranga kabla ya wiki nne,

Huharisha mharo mweupe, Pata vifaranga kutoka kwenye shamba abalo halina viashiria vya ugonjwa

- **Kipindupindu cha kuku (fowl cholera)**

Kinyesi cha kuku ni njano

- **Coccidiosis**

Mwanzo kinyesi cha ugoro na baadae huharisha damu iliyo changanyika na kinyesi

- **Mdondo (Newcastle)**

Kuku hunya kinyesi cha kijani sio kila kijani ni Newcastle unatakiwa kuambatanisha na dalili nyingine za ugonjwa pia kutazama idadi ya vifo bandani.

- **Typhoid**

Kinyesi cheupe, kinagandia sehemu za nyuma kwa vifaranga au hulowana sehemu za haja

Dawa ni Eb3, Trimafarm, Enrovet, Gnadexil, Limoxin

- **Gumboro**

Huathiri zaidi vifaranga wa wiki 1-3 Kinyesi huwa ni majimaji meupe Kuku wanatakiwa kupewa chanjo.siku 14-28

- **Mada kuhusu matumizi ya dawa kwa kuku**

Kitu cha kwanza ieleweke kwamba dawa sio kinga ila ni tiba ya ugonjwa ambao unakua umeshatokea kwa hiyo ni muhimu kuwapa kuku chanjo za magonjwa kwa kuzingatia ratiba sahihi ya chanjo. Chanjo pia kama haitahifadhiwa katika mazingira sahihi au kutumiwa kwa namna sahihi ubora wake hupungua hivyo ufanisi wake kukinga ugonjwa hupungua vilevile.

**Vitu sahihi kuvijua kabla hujatumiwa dawa yeyote**

- Hakikisha umefahamu ugonjwa upi unaoutibu.
- Hakiksha unajua ugonjwa upo katika level/stage ipi.
- Hakikisha umefanya uchunguzi juu ya magonjwa mengine yanaohusiana na ugonjwa husika
- Ni muhimu zaidi kufahamu umri wa kuku wako na kuchagua dawa sahihi kulingana na umri.
- Hakikisha unafahamu level ya uzalishaji na muda kabla ya kuchagua utumie dawa ipi.

Mara nyingi kuku akiumwa ugonjwa mmoja huongeza uwezekano wa kuumwa magonjwa mengine, hivyo ni muhimu kufanya uchunguzi mzuri na kabla ya kufanya maaumuzi ya kutumia dawa.

Dawa zinatofautiana level/nguvu na ufanisi kutoka kundi moja la kuku na lingine au kutoka Kwa mfugaji mmoja na mwingine kwa kutegemea aina ambazo zimeshatumika mwanzoni. Mfano; Dawa hiyo hiyo moja Kwa mfugaji mmoja inakuwa na ufanisi mkubwa na Kwa mwingine isitibu kabisa lakini ugonjwa uleule. Hii inatokana na matumizi ya dawa zingine yaliyokwisha tumika kabla Kwa kila mfugaji.

### **Kutoka na kugunduliwa na kutengenezwa dawa zimewekwa katika makundi manne**

>Kundi la Kwanza zilianza 1940's

>Kundi la pili 1970s'

>Kundi la tatu 1990's

>Mpya.

Sasa kwenye kutibu ukianzia dawa za kundi la tatu au la nne, Zitatibu vizuri Mara ya Kwanza lakini baada ya apo Kama zikiwa na usugu huwezi tena kutibu Kwa kutumia makundi mengine yote.

Lakini Kama ulikuwa unatumia kundi la Kwanza, ikiwa sugu unaenda la pili Ivo ivo mpaka kundi la mwisho. Ufanisi kwenye dawa unategemea hali katika banda lako hsifanani kwa wafugaji wote.

Baada ya kuwatibu kuku Kwa dawa haimanishi dawa itazuia wasiambukizwe tena ugonjwa, kama viini vya magonjwa vitaachwa katika mazingira ya banda lako mara tu baada ya kumaliza dozi wata ambukizwa tena na kuumwa tena, matibabu lazima yaambatane na hatua za kuzuia maambukizi mapya ikiwemo kuondoa sababu za maambukizi.

Tofauti na hivyo utatumia dawa watapona, utatumia tena, kutibu inakuwa ni Kama kulishia chakula.

Mpaka itafika muda utakuwa umehalibu maini ya kuku kutokana na matumizi ya dawa hapo hutapata faida.

Kwa kuku ambao wanakua kwa muda mrefu kama chotara, kuku wa mayai na wakiyenyeji ni vema wakiwa wadogo dawa zenye zitumike kuanzia kundi la Kwanza kuelekea linalofuata, Kwa kufuata dozi sahihi Kwa ugonjwa sahihi tofauti na ivo endapo wataugua tena hautakua na dawa mbadala.

### **Mfano kwa dawa za mafua**

Mfano namna ambavyo mafuaa yanaweza kutibu Kwa kufuanda mtililiko wa kundi la madawa

- Fluban/flutan
- Tylofarm
- Tylocox
- Enrovet

### **Coksidiosi /kuhara damu**

Kwa kua huu ugonjwa umekua ukiwasumbua sana wafugaji cha muhimu zingatia mazingira yako yawe makavu muda wote ili kuzuia huu ugonjwa usitokee.

Ni vema kama utataka kukinga, Utumie Agracox kwa sasa na kutibu uanze Amplorium/Vitacox/Trisul

Esb 3 iwe ni chaguo la mwisho kabisa.

### **Typhoid**

Hii pia ni changamoto kubwa kwa wafugaji walio wengi, cha muhimu hapaa kuku wapewe maji na chakula kisafi ambacho hakina uvundo

Matumizi ya dawa kwa kuku wadogo kabisa unaweza kuanza na dawa zenye sulphur zinazotibu huo ugonjwa

Unaweza kuanza na

- Trimafarm

- Esb3
- Doxcol kwa kuku wadogo ambao hawatagi

Kwa wanaotaga unaweza kutumia dozi salama zisizo na salfa kama

- Ganadexil. □ Enrovet
- Limoxin

Wakati mwingine kuku wanaumwa ugonjwa zaidi ya mmoja ambayo inatumia dawa zinazo kinzana katika kufanya kazi Katika hali kama hii inabidi ujitahidi kujuaa Kati ya hayo magonjwa upi inapelekea kifo Kwa haraka na matatizo makumbwa zaidi ndio ambao inabidi kuanza kuutibu.

### ➤ **Mada kuhusu minyoo kwa kuku**

Minyoo ni viumbe hai ambao huishi kwa kutegemea uwepo wa kiumbe mwingine kwa malazi na chakula, Kwa kuku minyoo ipo ya aina nyingi, ipo ya duara, ipo ya bapa ambayo ni mirefu sana ikiwapata kuku kupotea huchukua muda mrefu sana.

### **Chanzo cha minyoo**

Kuku kula chakula kichafu hasa kilicho changanyika na kinyesi hapa hasa kama unachanganya kuku wakubwa na wadogo madhara huwa endelevu bandani usipokinga.

Kuku wanao zunguka nje, kunywa maji yaliyotuama au maji yaliyokaa kwa muda mrefu pia kuparua mabaki yenye mazalia au mayai ya minyoo

### **Dalili za minyoo**

- Upungufu wa hamu ya kula
- Kupungua kwa utagaji
- Kupungua uzito
- Minyoo huonekana kwenye kinyesi
- Kuku kudumaa

Kwa kawaida minyoo huwa na mzunguko wao kuanzia

- Yai,
- Lava,

- Pupa ,na
- Mnyoo mkubwa

Hivyo minyoo ikiingia Kwa kuku huchukua muda wa wiki zaidi ya mbili kukua kufikia minyoo kamili

Kuku akishapata minyoo wakubwa hapa ndipo tatizo huanzia kwani mahai hutagwa kwa wingi na hutolewa kwa njia ya kinyesi na kuwafikia kuku wengine hivyo kama hatua za maksudi hazitachukuliwa ndani ya muda wa wiki 4 tangu minyoo kuingia bandani asilimia kubwa ya kuku watakua na minyoo

### **Kuzuia**

- Hakikisha mazingira yako ni salama na safi muda wote yasiyo maji yenye kutuama wala matope yanayo kuwepo kwa muda wote kuzunguka mahali kuku wanapoishi.
- Kuku wasile kinyesi
- Usichanganye kuku wadogo na wakubwa

### **TIBA**

Kitaalamu zipo dawa nyingi za minyoo ambazo kwa ratiba iliyo zoeleka hutakiwa kutolewa na kurudiwa kila baada ya miezi mitatu. Tatizo limekuja ni upi wakati sahihi wa kuanza dozi ya minyoo madaktari bobezi wa kuku wanashauri dawa za awali za minyoo zitolewe baada ya miezi miwili.

Inashauriwa kwa sehemu zenye maji yasiyo salama mfumo wa utoaji dawa za minyoo kwa Mara ya kwanza unatakiwa uwe wa kurudia kila baada ya wiki 2 rudia awamu tatu mfululizo.

### **Kwa nini irudiwe unapoanza dozi**

Dawa za minyoo hushambulia hatua mbili za ukuaji wa minyoo, ambazo ni minyoo wakubwa na wale wanaofuata kwa ukubwa ila haziathiri hatua za mayai na Lava ,hivyo ukiwapa dawa kwa kurudia kila baada ya wiki mbili Mara tatu mfululizo hii itapelekea hata yale mayai yatakua yamegeuka na kuwa minyoo wakubwa hivyo dawa itawaua na kupunguza tatizo kwa 75-85%.

Kusubir kuwapa kila baada ya miezi mitatu bila kufanya hizo hatua zilizolekezwa utakua unapunguza idadi ya minyoo na wakati mwingine minyoo itazidi na haitasikia dawa,

## **Matibabu**

- Ant worms.
- Piperezine.
- Albendazole.
- Ascarex
- Levamizol

## **Njia rahisi ya kutibu minyoo**

Awamu ya kwanza ya kuwapa dawa,

- Baada ya miezi miwili, dozi siku 1-2
- Rudia baada ya wiki 2 dozi siku 1-2
- Rudia baada ya wiki 2 dozi siku 1-2

Ukimaliza hapo wape dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu kuku wako watakua salama na huru dhidi ya minyoo

## **Zingatia**

- 1) Maji safi.
  - 2) Chakula safi.
  - 3) Banda safi.
  - 4) Fuata ratiba sahihi ya dawa hasa kila baada ya miezi mitatu.
- **Chawa, utitiri na viroboto**

Hawa ni wadudu ambao hupatikana kwenye mazingira aishipo kuku, kwa pamoja wadudu hawa hunyonya damu kwa kuku na kuua kuku hali ikizidi bandani.

## **Chanzo cha wadudu**

- Uchafu kwenye mazingira
- Uwepo wa wanyama wengine kama mbwa na panya



- Kuku wageni kuingia shambani
- Mipasuko kwenye banda

Zipa njia nyingi za kuzuia na kuondo wadudu hatari kwa kuku katika mazingira , miongoni mwa njia hizo ni kama zifuatazo

- Nyunyizia majivu, Chokaa na dawa za kuua wadudu kila usafishapo banda.
- Badilisha matandiko ya kuku pindi wadudu watakapo jitokeza
- Choma au fukia mabaki ya mayai baada ya kuku kutotoa
- Tumia dawa za kuua wadudu za kupulizia mfano Akheri powder

### **Dalili za kuku walioshambuliwa na wadudu**

- Ngozi nene, ngumu yenye magamba
- Kuku hujikuna
- Kuku wanaonekana kwenye mwili wa kuku
- Mnyoya kucha chamaa
- Kukosa hamu ya kula
- Kupunguza kula
- Rangi ya upanga hufubaa kuashiria upungufu wa damu **Hatua za**

### **kuchukua**

- Safisha vyombo vya chakula
- Watenge kuku wageni kabla ya kuwachanganya kwenye kundi
- Fanya usafi wa banda la kuku kabla na baada ya kutoa kuku kwa dawa
- Fuata ushauri kutoka kwa wataalamu wa mifugo
- 

### **Mada ya 5: Chanjo za kuku**

Kuna aina tofauti za magonjwa kama magonjwa ya virusi, magonjwa ya bacteria na magonjwa ya kupe/viroboto na minyoo

**5.1.** Magonjwa yanayo sababishwa na virusi hayatibiki hivyo mfugaji nivema ukawachanja kuku wako kwa moja ya mifumo ifuatayo

- Chanjo kipindi kifaranga akiwa ametotolewa day old chick/hatchery achanjwe
- Chanjoya Marekskwa kuku wa mayai (Sasso, Kuloirer, pure layers Breeder isipokua pure broilers
- Chanjoya Infectious Bursal Disease/Gumboro
- Chanjoya Infectious Bronchitis na Newcastle/ kideli/ mdomo

### **5.2. Mfumo wa kwanza wa chanjo**

- Siku ya kumi chanjo ya kideli/naIB
- sikuya 18 chanjo ya gumboro/Ibd
- sikuya 28 chanjo ya kideli/newcastle
- sikuya 30 chanjo ya ndui/fowl pox
- Kila baada ya miezi mitatu au wiki ya 12 wape chanjo yakideli/ Newcastle hadi pale utakapo watoa kuku wako
- Kila baada ya miezi mitatu wape dawa za minyoo

### **5.3. Mfumo wa pili wa chanjo**

Siku ya saba chanjo ya kideli/newcastle

Sikuya 14 chanjo ya gumboro/ibd

Sikuya 21 chanjo ya newcastle/kideli

Sikuya 30 chanjo yandui/fowl pox

Kila baada ya miezi mitatu rudia chanjo ya Newcastle mpaka utakapo watoa kuku

Kila baada yamiezi mitatu wapedawa za minyoo wape dawa ya minyoo kwa mara ya kwanza wakiwa na umri wa miezi miwili

#### **5.4.Mambo ya kuzingati wakati wa kuchanja kuku**

Siku ya kuchanja kuku hakikisha kuku wametolewa maji asubuhi kabisa na uwanyime maji kwa masaa yasiyozidi mawili.

Vyombo vyako vya kuwekea chanjo vioshwe vizuri kwa majisafi.

Maji ya kuwekea chanjo yawe masafi na yachanganywe na Coper au Chlorex blue ili kuondoa chlorine ya kwenye maji kufanya chanjo iwe na nguvu.

Chanjo iliyotunzwa kwenye friji ichanganywe kwenye maji kutokana na wingi wa kuku mara nyingi kopo moja la chanjo nikwa kuku 500-1000 kwa hio angalia una kuku wangapi alafu wachanganyie maji watakayo weza kumaliza yasiyopungue lita 5-20 kwa chupa ya chanjo.

Wape maji yenye chanjo kwa muda wa saa1 hadi masaa mawili alafu toa maji yenye chanjo.

Dakika tano baada ya kuweka chanjo angalia kama kuku wote/vifaranga wote wame kunywa maji yenye chanjo kwa kutazama midomo yao itakua na rangi ya maji yenye copper/Cevamune

Kama kuna kifaranga hajanywa maji yachanjo mnyweshe kwa kijiko, au syringe (bomba la sindano)

#### **Zingatia**

Kwa kuku anaetaga usimtibu kwa dawa zenye mchanganyiko wa salpha, kwani hushusha utagaji au kukata utagaji kwa muda fulani hivyo ni vema kutumia dawa mbadala ya kutibu ugonjwa husika.

## **Mada ya 6: Soko la kuku na mazao ya kuku**

Kutokana na malalamiko ya wafugaji wengi wa kuku kuhusu ukosefu wa soko la uhakika la kuku na mazao yake kama nyama na mayai, yafuatayo yanapaswa kufanyika. Kabla ya kuanza mradi mfugaji anatakiwa afanye uchunguzi wa soko la atakacho zalisha

- Kwanza ajue mazingira yanayo mzunguka au atakapo fugia yanahitaji nini, je ni nyama au mayai kama ni mayai je ni aina gani ya chotara au kienyeji au ya kisasa ndipo aamue kuanza uzalishaji,
- Kama sio hivyo mfugaji ajue kama oko lake litakua mbali ni vipi atasafirisha na kutunza bidhaa zake atakazo zalisha akizingatia inabidi apatefaida.
- Kutazama upatikanaji wa malighafi atakazo tumia wakati wa uzalishaji, ziwe ni kwagharama ya chini
- Anapaswa ajue wapi hasa na nani atakua mteja wake mkuu na atapambana vipi na changamoto zisizo zuilika

## **Suluhisho**

Kuteka soko ni lazima mfugaji azalishe bidhaa zenye ubora wa hali ya juu, kama ni nyama iwe yenye sifa zote kwa mlaji na kama ni mayai yawe mazuri (Makubwa, yenye kiini cha njano, masafi, ganda lenye mvuto).

Mfugaji anapaswa kuwa mbunifu wa jinsi ya kuliteka soko la mahali alipo mfano asogeze huduma kwa mteja kumletea mayai au nyama pale anapo patikana mteja, kama ni nyama aiandae kabisa kupunguza usumbufu kwa mteja

Kwa ufugaji wa kuku wa nyama/broiler unaweza kufuga kwa kulenga misimu mfano sikukuu za kitaifa, za kidini, au sherehe mbalimbali unajua tarehe mfano kuna tukio flani.

Kutokana na mazingira wafugaji mlipo, mnaweza kuanzisha Umoja kama Mkoa, wilaya, kata, tarafa ambapo mtakua mnakutana na kuunganisha nguvu ya kusafirisha na uuzaji wa bidhaa zenu pia kupanga bei za mazao ya kuku kutokana na mabadiliko ya garama za uzalishaji

Kuendelea kufumbua macho zaidi sehemu mbali mbali kujifunza ni kwa namna gani wanapata masokonakupambananachangamoto za soko

Mradiukikuamnawezakuanzisha vituo vya kuuzia bidhaa zenu mikoani na hiyo itasaidia mtambulike kama wauzaji wa bidhaahusika.

Kama mazingira uliyopo yana ruhusu, uza nyama ya kuku kwa kilo usiuze kuku akiwa mzima utapata faida na hili litafanikiwa zaidi Mara baada ya umoja kuanzishwa na kulitetea kwa nguvu.

## **Mada ya 7: Stress/msongo wa mawazo kwa kuku**

Afyaya kuku kwa ujumla inaweza kutegemeana maisha yao ya kila siku. Mawazo yanaweza kuathiri kuku mmoja mmoja au kundizimabandani, lakini pia inaweza kuathiri kwa muda mrefu ambayo hupelekea kupungua kwa uzalishaji wa mayai, kuku kudumaa, kuku kula mayai yao wenyewe, natabia zote zisizo za kawaida

Asilimia kubwa sisi wafugaji tunapooni mabadiliko katika mabanda yetu ya kuku moja kwa moja huwa tunatafuta mchawi ni nani bila kukumbuka stress. hali inayopelekea kuwapa kuku madawa tofauti na tatizo bila kupata suluhu hapo utasikia duka Fulani dawa zao si bora.

## 7.1. Kuku kwa asili

Hawajaitwa 'kuku' bure! Kwa asili wao ni waoga. Ndege wengi wanaonekana kuogopa vivuli vyao wenyewe, na wanaonekana kuwa natabia yakuruka kila wakati wana posumbuliwa.

Hofu itaunda mafadhaiko au msongo, na hi inaweza kusababisha malalamiko na magonjwa ambayo hayange athiri kuku wako ,mafadhaiko/stress husababisha pH kwenye utumbo kupungua na hii inaunda bakteria ya 'gramu hasi' ambayo kusababisha ugonjwa.

## 7.2. Sababu zinasababisha la kuku mfadhaiko (stress) kwenye banda nikama zifuatazo

### 7.2. A.Mashambulio ya wanyama wakali au binadamu

Hapa wanyama wakali tunaongelea wanyama kama nyoka, mbwa, paka nk. Wanapoingia bandani husababisha madhara kwa baadhi ya kuku hadi kuwajeruhi kabisa hii husababishia kuku msongo wa mawazo hadi kupelekea kuathiri mfumo wa maisha ya kila siku ya kuku.

### 7.2. b.Wadudu

Wadudu kama chawa, viroboto, papasi na husabababisha ghasia kwenye banda la kuku wao huwapa kero kubwa kuku wako hasa nyakati za usiku na kusababisha msongo wa mawazo kwa kuku na hii inaweza leta shida zaidi kwenye kuku wa mayai hapa utagaji huwa unapungua kwa kasi sana hadi kufikia asilimia 80-90.

### 7.2. c.Joto la juu au la chini

Tofauti kubwa katika joto zinaweza kusababisha shida kubwa. Hali ya hewa baridi sana wakati wa usiku, wakati hali ya joto inapungua chini ya sifuri, ni hatari kwa kuku, haswa kwa vifaranga.

Kwa kuku wa mayai inasababisha mporomoko wa uzalishaji wa mayai kwa asilimia hadi 80.

#### 7.2.c.Wakati wa kuzaliana ( kupandana) navifaranga pia

Kuhakikisha mahitaji ya lishe yanatimizwa katika kipindi hiki ni muhimu sana tena, hakikisha kila wakati unawapa maji safi, na kuongeza vitamin itasaidia ndege kupitia wakati huu. Kupandana nisababu dhahiri ya mfadhaiko kwa sababu ya nguvu na vitendo vya ghafla

#### 7.2.d.Mabadiliko ya mazingira

Mabadiliko ya mazingira kwa kuku, kama vile kuhama banda au kuwa na muhudumu mpya ni wakati mwingine mgumu sana kwa kuku. Ili kuhamisha ndege kwenye banda jipya, unapo wahamisha Weka mbali kitu chochote kinachoweza kuwafanya kuwa na hofu, kama vile mbwa watu au kelele nyingi, Daima hakikisha kuku mpya na wa zamani hawaishi pamona kwenye banda jipya kwani umevu unaweza kuwa na athari kubwa.

### 7.3.Matibabu

7.3. 1.Kuku wanapotoka kwenye ugonjwana kupata matibabu huwa na msongo wa mawazo hivyo unatakiwa kuwapa ant stress ili kuwarudisha kwenye haliyaoyakawaida

#### 7.3.2.Kuoga dawa

Wengi wetu tumezoea kuwaogeshwa kuku wetu dawa hasa tunapogundua kuwa wana shambuliwa na wadudu ndani ya manyoya yao, hivyo baada ya kuwaogeshwa dawa unatakiwa kuwapa ant-stress ili kuwaepusha na msongo wa mawazo.

#### 7.3.3 Kusafiri na kelele nyingi

Kusafiri kwa gari kunaweza kuwa shida kelele iliyoundwa na gari pamoja na harakati zisizo za kawaida ambazo kuku hawajazoea . Kusafiri katika sanduku lenye hewa nzuri ni njia bora ya kusafirisha, na hii pia itasaidia kuku kupumzika. Ila baada ya safari mpatie glucose na anti stress

#### 7.3.4.Maonyesho

Maonesho kama nane nane au mengine yoyote huwasababishia kuku msongo wa mawazo hivyo unashauriwa unapotoka kwenye msonesho uwape kuku wako anti stress ili warudi kwenye hali yao ya kawaida.

### **Mwisho**

kuku ni kama wanadamu au viumbe wengine, lazima kukabiliana na mafadhaiko/stress kila siku ya maisha yao. Hivyo unashauriwa kuwalea katika misingi ya kitaalamu ili kunufaika naufugaji.

Nb: Unapo ona mabadiliko yauzalishaji au ukuaji bandani kwako kumbuka pia na msongo wa mawazo, endapo hautopata suluhisho la kushuka kwa uzalishaji au ukuaji wa kuku wako ili kuepusha gharama za matibabu yasiyo ya lazima



## **Mada ya 8: Vifaa vya kulishia na kunyweshea maji**

Kuku wanahitaji vifaa vya kutosha vya kunywa maji na kulia chakula ili wasigombanie nahivo kupelekea kudonoana

Vifaranga wadogo unaweza kuanza kuwawekea chakula kwenye mifuko/salfeti au magazeti na uyabadilishe haraka yatakapo chafuka kila siku kwa muda wa siku 5 za kwanza

Baada ya hapo anza kuwazoesha kuweka chakula kwenye vilishio

Kwa vifaranga tumia vinywesheo vidogo iliwaweze kupata maji kwawingi

Hakilikisha kadri kuku wanavokua unanyanyua vinywesheo vya maji kulingana na umri wa kuku iliwasimwage maji bandani kuzuia magonjwa

### **8.1. Drinkers au vinywesheo vya maji**

- Kuku wakiwa wadogo drinker kubwa 1 kwa kuku 25
- Kama utatumia drinker ndogo drinker 1 weka kuku 10-15



## **Vyombo vya kunyweshea maji kuku**

### **8.2. Feeders au vyakuwekeachakula**

- Kwa kuku wadogoukitumiazilekubwa 1 kwa kuku 25
- Wakiongezeka umri kuwa wakubwa feeder 1 kwa kuku 1015
- Na hapa ukiona wanagombea sana chakula kuwa vyombo ni vichache unaweza ongeza idadi ya feeders na drinkers.



## **Vyombo vya chakula**

### **Mada ya 9: Makala juu ya ulishaji au uchanganyaji wa chakula**

Kwanza mfugaji anapaswa kujua aina ya kuku na umri wao kabla ya kuanza kufikiria kutengeneza chakula, kwa mfano anataka kutengeneza chakula cha kuku wa mayai au wanyama , na hatua ipi ya ukuaji je ni starter au ni grower au nifinisher

Kitu kingine mfugaji anapaswa kuangalia gharama ya malighafi mahala alipo, na urahisi wa upatikanaji kutumia malighafi ambazo utazifata mbali kutaongeza gharama ya ufugaji

Mfugaji anapaswa kujua uhitaji wa virutubisho kwa kundi na aina husika ya kuku kabla hajaanza kutengeneza chakula

Kama mfugaji atakua ameyafahamu hayo ndipo aanze kutengeneza chakula, ushauri kama inawezekana ukichanganya chakula peleka maabara kuhakiki uwepo wa virutubisho vyote kulingana na kundi la kuku.

#### **9.1.Virutubisho muhimu kwa kuku**

Kuku ili akue vizuri na kutaga vizuri anatakiwa kupewa chakula chenye mchanganyiko ufuatao

- Protein
- Wanga au nafaka
- Vitamins
- Madini
- Mafuta

**a. Starter**

Unapotengeneza chakula cha starter kwa broiler

Energy au nafaka iwe na 60%

Protein 40% ambapo ukipima protein kwenye chakula maabara inabidi iwe 19-22 %

**b. Grower**

Energy au nafaka 65%

Protein 35 na ukipima ikuletee mchanganyo wa protein wenye 1819%

**c. Finisher**

Energy/ wanga inabidi iwe 70-75%

Protein 25-30% ambapo ukipima protein kwenye chakula inatakiwa kuwa 17-18%

Kwa mwongozo huo kiwango cha nafaka au wanga kinaongezeka kadri kuku wanavozidi kukua wakati kiwango cha protein kinakua kinapungua, kama utafanikiwa kutengeneza chakula chako kwa mfumo huo kuku wataenda vema

Chakula cha kuku ni lazima kiwe na madini, premix na vitamins

**9.1.2. Madini** kama calcium na phosphorus yanapatikana kwenye Chokaa, DCP, Mifupa, maganda ya konokono na vingine

**9.1. 3.Vitamins** zaweza kuwa za kikemikali/Artificial au unaweza kuweka premix ambazo zinakua pia na vitamins

**9.1.4. Protein** unaweza tumia, Soya meal, Alizeti, Mashudu ya pamba, Dagaa, Uduvi, Hii itategemea wewe upo eneo gani na utaangalia urahisi wa upatikanaji

**9.1.5. Energy/Nafaka** unaweza ukatumia , mahindi yaliyo parazwa, pumba ya mpunga, pumba ya ngano , pumba ya mpunga , mtama

**9.2.Formula ya kuku wa kienyeji**

Na	Aina ya chakula	Sterter(kg)	Grower(kg)	Layers(kg)
1	Mahindi paraza	8	8	8
2	Pumba za mahindi	20	20	20
3	Mashudu ya alizeti	7	7	10
4	Unga wa dagaa	6	6	3.5
5	Chokaa ya mifugo	2	2	4
6	Chumvi	0.25	0.25	0.25
7	Soya iliyo barazwa	3	3	-
8	Unga wa damu	1	1	-
9	Premix	0.5	0.5	0.5
10	Egg booster	-	-	0.5
11	Unga wa mifupa/Dcp	1	2	4

### **9.2.1.Unacho takiwa kufanya wakati wa kuchanganya chakula**

Hatua ya kwanza andaa sehemu safi utakayo changanyia chakula, unaweza kutandika turubai ili chakula kiwe rahisi kuzoleka

Mbili vichanganye vyakula vyenye uwiano mdogo pamoja kwanza mfano lysine, methionine, chumvi, premix, Dcp, chokaa

Baada ya hapo anza kuongeza vyakula vyenye ujazo mkubwa kidogo kidogo kama mahindi paraza, pumba, soya, alizeti n.k

Hakikisha huo mchanganyo wa awali umechanganyika vema unaweza kutumia spedi au mikono kutokana na kiwango cha chakula unacho kiandaa

Ukijiridhisha kuwa mchanganyo wako upo tayari, mwaga juu yake vyakula vyote vilivyo salia kisha endelea kuchanganya kwa kugeuza geuza mpaka pale utakapo ona chakula kime changanyika kwa usahihi na msawazo wa virutubisho

### **Zingatia**

Vyakula kama Pumba za ngano au mahindi, Alizeti au Soya zinatakiwa kuchekechwa ili kutoa aina zote za vyuma au mawe magumu ambayo yanaweza kuleta athari kwa afya ya kuku

### **Mada ya 10: Mwanga kwa kuku**

Mwanga Ni kiambata muhimu Sana Kwa ukuaji Na utagaji Kwa kuku, mwanga hupelekea kuku kupevuka/maturity kwa wakati. Mwanga ni muhimu kwa kuku aina zote na hasa kwa kuku wa mayai ni vema sana kuzingatia ratiba ya mwanga kwa kuku

Mfano wa kuku wa mayai, Hy-line, Bvon brown, Red Island, Isa brown, Lohman brown na wengine wengi.

Mwongozo huu ni maelezo sahihi ya kufuata kulea kuku tangu akiwa kifaranga mpaka akianza kutaga, na masaa hutofautiana kwa kila wiki.

Njia rahisi ya kuendana na mwanga kwa kuku ni kuzima na kuwasha taa kwa muda sahihi kulingana na hatua ya ukuaji wa kuku wako.

Kuku wakianza kutaga wanatakiwa kupewa jumla ya masaa 16 mpaka watakapo fikia umri wa kutolewa bandani.

### **MWONGOZO WA MWANGA**

Wiki ya 1 masaa 22-23

Wiki ya 2 masaa 19-20

Wiki ya 3 masaa 17-18

Wiki ya 4 masaa 15-16

Wiki ya 5 masaa 14-15

Wiki ya 6 masaa 13-14

Wiki ya 7 masaa 13

Wiki ya 8 masaa 12

Wiki ya 9 masaa 12

Wiki ya 10 masaa 12

Wiki ya 11 masaa 12

Wiki ya 12 masaa 12

Wiki ya 13 masaa 12:30

Wiki ya 14 masaa 13

Wiki ya 15 masaa 13:30

Wiki ya 16 masaa 14:30

Wiki ya 17 masaa 15:30

Wiki ya 18 masaa 16

Kuku wapewe masaa 16 ya mwanga tangu pale watakapo anza kutaga mpaka utakapo watoa bandani.

**NB: Mwanga unaweza kucheleweshwa au kuwahishwa kwa kuangalia ukuaji/kukomaa kwa kuku na kwa kuzingatia uzito wao.**

Walishe kuku wako kwa usahihi ili wafikie uzito unaotakiwa kwa wakati nah ii itawawezesha kuanza kutaga mayai kwa wakati.

## **Mada ya 11: Hatua za kulea vifaranga**

Andaa banda lako liwe safi na lililo puliziwa dawa kama V-RID au TH4 pia mlangoni weka maji ya kukanyaga yenye dawa ya Farm guard

Kisha andaa maranda safi yasiyo na vumbi....weka ujazo wa kimo cha 5cm kwenye banda

Andaa sehemu ya kulelea vifaranga/brooder kama mzunguko wa singbod au mabox ikate urefu au kimo cha 30 cm au 40cm

Tandika mifuko au magazeti juu ya maranda hii itasaidia kuku kutambua chakula mapema

### **11.1. Masaa mawili kabla yakuweka vifaranga**

Weka maji kwenye drinkers na chakula/Starter... sambaza kwenye mifuko au sahani za kulishia vifaranga



Wawekee chanzo cha joto Vyungu taa za watt 200 kati ya hizo utakacho weza kukipata masaa 12 kabla ya kuleta vifaranga kwa sehemu zenye baridi

Wape vifaranga Neoxychick kukausha vitovu kama watakua wamechoka wachanganyie GLUCOVET 11.2.Kwa broilers/

### **Kuku wa nyama**

Siku ya 7 wape chanjo ya Newcastle

Siku ya 14 chanjo ya gumboro

Siku ya 21 Newcastle

### **11.2.Kwa layers chotara na kuku wa kienyeji**

Siku ya 7 chanjo ya Newcastle

Siku ya 14 gumboro

Siku ya 21 Newcastle

Siku ya 28 chanjo ya gumboro (optional inategemea umechukua vifaranga kampuni gani)

Siku ya 30 chanjo ya ndui

Kilaa baada ya miezi 2-3 rudia chanjo ya Newcastle Kila

baada ya miezi mi 3 wape dawa za minyoo.



## Sehemu ya kulelea vifaranga/Brooder

### 11.3. Utambuzi wa hali ya joto bandani

**Baridi:** Vifaranga watakusanyika pamoja na kulliana, pia vifaranga husogea karibu na chanzo cha joto, suluhu yake ni kuongeza chanzo cha joto bandani

**Joto kubwa:** Vifaranga wataenda mbali na chanzo cha joto, watatanua midomo na mabawa ili kupunguza joto, suluhisho punguza chanjo cha joto

**Joto sahihi:** Vifaranga watasambaa bandani vizuri na wataendelea kula na kunywa maji nahii hupelekea kuku kukua kwa uwiano.

**Upepo:** Vifaranga watakimbia na kuzunguka zunguka bandani, na kukusanyana upande ambao upepo haupo kwa wingi.

## Mada ya 12: Uoteshaji wa majani

a) Hydroponic fodder

- Unachukua aina yoyote ya nafaka mfano. Mtama, mahindi au uwele

- Unaosha nafaka utakayo amua kutumia kwa jiki kama inapatikana
- Baada ya hapoo unayatoa kwenye maji uliyokuwa unasafisha hizoo nafaka
- Unaloweka nafaka uliyoisafisha kwa maji safi kwa muda wa masaa 12
- Baada ya masaa 12 nafaka yako itakuwa imeshapata maji ya kutosha
- Unaziweka nafaka zako kwenye chombo ambacho kinapatikana sana sana wanatumia trey maalum za kuwekea ambazo zipo kama sahani au sinia unazifunika kwa nylon yoyote lakini sana sana wengi wanatumia gazeti au nylon nyeusi
- Unaziweka kwenye chumba ambacho hakipitishi mwanga kwa muda wa masaa 48
- Baada ya masaa 48 ukienda kufunua utakuta nafaka uliyochagua imeota nyuzi nyuzi nyeupe utatakiwa utoe trey za hiyo nafaka uliyochagua na kuweka sehemu iliyotengenezwa rasmi kama kichanja tray zina beba gram 200-500...inategemeana na ukubwa
- Utatakiwa uwe unamwagilia maji kila maraa
- Baada ya siku nne kuanzia ile siku uliyoweka kwenye kichanja utatakiwa uwape kuku wako kwasababu itakuwa tayar kwa ajili ya matumizi na baada ya siku saba unaweza kuwapa wanyama wengine kama sungura, ng'ombe, mbuzi, nguruwe
- Majani haya huweza kupunguza kwa kiasi matumizi ya chakula pia huwa ni muhimu kwa kuongeza vitamin kwa kuku na kupelekea afya bora.



## **Majani yaliyooteshwa kwa muda mfupi.**

### **b. : Uoteshaji wa Azolla**

Azolla ni majani/magugu ambayo huota sehemu yenye maji kwa wingi. Hutumika kwa chakula cha mifugo wa aina mbalimbali, mmea huu pia umekua ukitumika na wafugaji wengi kama chakula mbadala kwa kuku,

Azolla inaweza kuliwa na kuku ikiwa mbichi/fresh au ikivunwa na kuanikwa kisha kuchanganywa kwenye chakula cha kuku.

### **Sifa za azolla**

- Kiwango kikubwa cha protini 19-30%CP.
- Crude fiber 15%
- Uwezo wa kutoa maotea kwa wingi ndani ya muda mfupi siku 310.
- Lysine 4-6%

### **Jinsi ya kuotesha**

Tengeneza bwawa kulingana na ukubwa wa eneo ulilo nalo kwa kujengea kwa tofali na cement au nylon sheet kuzuia upotevu wa maji. Kwenye dimbwi lako weka bomba dogo la kuruhusu maji kutoka pindi maji yatakapo jaa kuzuia upotevu wa azolla.

### **Faida za azolla**

- Ni rahisi kuzalisha
- Inazaliana kwa wingi
- Ina protini kwa wingi na vitamin
- Inapunguza gharama ya chakula



## **Bwawa la azolla**

### **Mfano**

- Upana mita 2 na urefu mita 3
- Kina/deep chenye 10-15 cm
- Weka mbolea ya ng'ombe ndoo moja kwenye bwawa lako
- Mwaga mbegu ya azolla mbichi bwawani ianze kuota
- una azolla iliyo tayari na kubakiza nyingine itakayo endelea kuongezeka kila siku bwawani
- Pindi azolla itakapo badilisha rangi kupoteza ukijani, ongeza mbolea ya ng'ombe itastawi vizuri

Ukivuna azolla wape kuku wako ikiwa mbichi au iliyo kaushwa kwa kuchanganya na chakula kingine.

NB: Bwawa kwaajili ya kuotesha azolla linatakiwa kujengwa eneo lisiloruhusu mwanga mkali wa jua kufika moja kwa moja bwawani, eneo linatakiwa liwe na kivuli au kutumia turubai maalumu (Shade net) la kuzuia mwangawa jua na kuruhusu 30% ya mwanga kuifikia Azolla.

## **Mada ya 13: Kuku kula mayai, kudonoana na kunyonyoka manyoya**

Tatizo la kuku kuwa na tabia zisizo faa/cannibalism limekua shida kubwa kwa wafugaji wengi wa kuku aina zote, ilaa limekua likijitokeza sana hasa kwa kuku wa mayai

Tatizo hili pia limekua likijitokeza kwa kuku wa rika tofauti tofauti. ilaa linazidi pale kuku wanapo anza kutaga mayai

### **13.1. Chanzo cha tatizo**

Kuku kuwa wengi kwenye banda dogo kuzidi uwezo wa banda kuhifadhi kuku

Kukosekana kwa vifaa vya kutosha vya chakula na maji pia kuku kukosa chakula cha kutosha

Upungufu wa protini, na madini kama calcium kwenye chakula cha kuku

Kuwa na idadi kubwa ya majogoo bandani kuzidi idadi inayotakiwa

Kuku kuchoka au kuzeeka pale muda wake utakapo kua umefika mwishoni

### **Suluhisho**

Kwa kuku anaekula mayai, mwongezee kiwango cha chakula chenye protein kwenye chakula kama soya meal na dagaa, pia mwongezee vitamins kuku wako atapunguza kula mayai pia waongezee kiwango cha mifupa au chokaa kwenye chakula chao,,kama utatumia magamba ya konokono hakikisha usalama wake maana wakati mwingine hupelekea Typhoid

Kwa kuku wanao donoana, weka kiwango sahihi cha vifaa vya maji na chakula, weka idadi sahihi ya kuku bandani wapate nafasi, wawekee majani muda fulani ili chakula kikiisha wawe busy kula wasipate muda wa kudonoana

Kwa kudonoana na kula mayai, endapo utatumia mbinu zote hapo juu na isisaidie njia ya mwisho kabisa ni kuwakata kuku midomo kwa kutumia kifaa maalumu cha kukatia midomo de-beacker...au

kuchoma mdomo kwa njia za kienyeji, baada ya kuwakata midomo wape chakula kingi na vitamins kwa wingi

Kwa kuku wanao nyonyoka manyoya, waweke jogoo kwa uwiano na tetea, jogooo mmoja kwa tetea 8-10, wape chakula chenye mchanganyiko wa madini ya calcium, zuia wadudu kama utitiri viroboto au kupe kwa kupulizia dawa ya Akheri powder au Paranex piaa usafi bandani uwe wakuridhisha.

Kikubwa cha kufahamu hapa ukifuatilia kwa makini hizi changamoto huwapata zaidi kuku ambao wafugaji hujichanganyia chakula chao, hivo ni vema ukachanganya chakula kutokana na uhitaji wa kuku na umri wa kuku na utumie formula sahihi ya mchanganyiko wa chakula



## **Kuku alie donolewa**

### **Mada ya 14. Nasaha kuhusu ufugaji wa kuku**

Ufugaji wa kuku unahitaji uelewa wa vitu vingi ili uweze kufuga jwa kukupatia faida ndani ya kipindi kifupi kutokana na mpango kazi, pia ufugaji kuku kiusahihi ni taaluma ambayo mfugaji anapaswa kuwa nayo ili kumuwezesha kutoa huduma stahiki kwa kuku waweze kumletea matokeo chanja katika ukuaji na uzalishaji wa mayai kwa wakati. Ufugaji wa kuku ni Zaidi ya kuwa na mtaji wa kuanzisha biashara, kwani unaweza ukawa na mtaji ila kama hutafuata taratibu na kanuni za ufugaji sahihi unaweza kupata mafanikio hasi.

## Mambo ya kuzingatia

- Utulivu wa akili na kufikiria kwa kina juu ya mradi kabla haujaanza uzalishaji, weka mpango lazi/plani ya ufugaji (business plan) itakayo kusaidia kujua gharama sahihi za uendeshaji na kiasi utakacho kipata kama faida baada ya kuuza mazao ya kuku.
- Kabla ya kuanza ufugaji ni wajibu kufanya uchunguzi wa changamoto za biashara ya kuku na jinsi ya kuzikabili pia kujifunza mbinu bora za ufugaji wa kuku
- Mfugaji anapaswa kufahamu mahitaji muhimu kwa kuku na aweza kuyatimiza ili kuku akue vizuri na aweze kuzalisha mayai mengi yenye ubora. Mfano Chakula bora na maji safi, Nyumba zahihi ya kuku, Uhuru dhidi ya magonjwa na stress/ msongo wa mawazo, kuku apate joto na hewa safi pia kuwe na mwanga wa kutosha bandani.
- Ufahamu kuhusu soko la kuku au mayai kwa eneo ulipo ili kufanya uamuzi aina ipi ya kuku uanze kufuga na utapambanaje pale gharama ya uzalishaji itakapo ongezeka.  
□ Usitatue changamoto za kuku kwa kuiga kutoka kwa mfugaji mwenzako bali watafute watalamu wa mifugo wakusaidie au mtu mzoefu sana wa mifugo hasa kwa maswala ya magonjwa hapa unao wajibu wa kuwafahamu wataalamu wa mifugo wanao kuzunguka.
- Uangalizi wa mara kwa mara wa kuku, kila siku asubuhi angalia mienendo na tabia zao kubaini kama kuna magonjwa
- Kwa usalama wa afya ya mlaji epuka kuuza kuku ambae umemchanja ndani ya siku chache au ambae yupo kwenye dozi za magonjwa
- Zalisha bidhaa bora za kuku kama mayai makubwa, masafi kiini cha njano pia nyama iwe yenye ubora wa kulizisha.



- Uwe na moyo wa uvumilivu pasipo kukata tamaa, uwe mjasiriamali utakae chukua changamoto na kuitatua ikuletee matokeo chanya baada ya muda Fulani.
- Kulingana na kanda na mahali mlipo undeni umoja ambao utawawezesha kufanya makubaliano ya bei za mauzo ya kuku na mayai kwa kutokana na mabadiliko ya gharama za uzalishaji
- Pia kuku ni vema wakauzwa kwa kilo kama ilivyo kwa nyama za mifugo mingine ifugwayo na isiyofugwa.
- Kuku ni idara pana hivyo kuteka soko inabidi ufanye utafiti wa haraka ili kukimbizna na hali iliyopo, jifunze namna bora ya kutengeneza chakula cha kuku kupunguza garama hasa kwa kununua mazao pindi yanapokua yanauzwa kwa gharama nafuu. Pia ukiwa na eneo kubwa ni vema ukafanya kilimo kwaajili ya mazao ya malisho kwa kuku.

### **Mada ya 15. kuhusu uwiano wa ukuaji kwa kuku/uniformity**

Msawazo kwenye ukuaji wa kuku/uniformity ni moja ya kitu muhimu sana kwenye ufugaji wa kuku ambapo mfugaji kwa namna yoyote unapaswa kuhakikisha kuku wanakua na uzito unao wiana ili kuepusha kuku kutofautiana sana muda wa kuanza kutaga.

Kuku wanaweza kula chakula cha aina moja, wakakaa banda moja na kutumia vyombo vya aina sawa lakini ukuaji wao uka tofautiana, hii ni kawaida lakini ni jukumu la mfugaji au msimamizi wa shamba la kuku kuhakikisha kuku wote wanakua kwa uwiano ulio ainishwa.

Kuku wanaweza kuwa kwenye banda lakini wakajigawa kwenye makundi matatu

- Uzito mkubwa/heavy weight
- Uzito wa kati/Medium weight
- Uzito mdogo/Light weight

Hii kwenye ufugaji sahihi hasa kuku wa mayai na nyama haitakiwi kwani husumbua wakati wa masoko na wakati wa kutaga.

### **Nini ufanye**

- Kwanza inatakiwa kujua aina ya kuku wako wanatakiwa kuwa na uzito upi angalau kwa kila wiki hii itakusaidia kujua kama kuku wako wanafuata ukuaji sahihi au hawa tofautiani,.
- Pili hakikisha kuku wako wanapimwa kwa kuchukua sampo kila wiki ili kubaini kama kuna makundi hayo matatu’
- Hakikisha kuku wanapata chakula cha kiwango sahihi, ikiambatana na idadi sahihi ya vyombo vya chakula na maji  
**Ikitokea wamepushana uzito nini ufanye**

Kwakua utakua umepima uzito wa kuku wako utatakiwa kuwatenga kuku kwa kufuata uzito wao/Grading; Hii itasaidia kupunguza kasi ya kuendeleza kizazi chenye mpishano mkubwa wa uzito **Mfano**

- Kuku anatakiwa awe na kilo 1-2 ndani ya wiki 12 Alafu ukakuta wengine wana gram 1500, wengine 1900, na wengine 2300, Hapa utatakiwa kuwatenga kwenye makundi yao ili wote wafikie uzito unaotakiwa’ Kwa wenye uzito mdogo, ukiwatenga fanya yafuatayo

1. Waongezee vyombo vya chakula na maji

2. Waongezee mwanga
3. Wape vitamins kwa wingi
4. Kama wataonesha kupanda uzito taratibu ongeza kiwango kidogo cha chakula
5. Waongezee eneo lao la kuishi Kwa wenye uzito wa kati
  - Hawa endelea na ulishaji sahihi ili wasipande wala kushuka kwenye kiwango cha uzito uliopangwa.
  - Wape mwanga sahihi
  - Chakula kiwango sahihi
  - Vyombo vya maji na chakula sahihi Kwa waliozidi sana uzito
  - Hawa nao wanatakiwa kurudi kwenye uzito unaotakiwa, hivyo chakufanya
  - Usiwapunguzie sana chakula, bali uwapunguzie masaa ya mwanga
  - Usiwape eneo kubwa sana la kuishi
  - Pia upunguze vifaa vya chakula ili wasiwe huru kula muda wote, huku ukizingatia kwamba hawataanza kudonoana.

Matokeo ya kufanya grading/kuwa tenga kuku kwenye makuindi yao

- Kuku wataanza kutaga bila kupishana sana
- Kuku watataga mayai yenye uzito/size moja
- Kuku watakua na rika moja kiumbo
- Kuku wanyama watakua na uzito unaowiana hivyo hawatakusumbua kwenye mauzo Sokoni

## **Mada ya 16. Matibabu ya kuku kwa dawa za asili**

Ipo mimea mbali mbali ambayo huwa tiba Kwa kuku na ndege wengine, hii ikitumika husaidia sana kupunguza idadi ya kuku wanao umwa pia kupunguza gharama za matumizi ya dawa za madukani. Katika kutibu mimea, au majani, magome, Matunda au Maua hutumika Kama tiba kwa kuku hasa kwa kuzingatia maelekezo sahihi ya matumizi ya dawa husika. **Mimea inayotibu maradhi ya kuku**

### **1. Mlonge**

Huu ni mmea ambao hupatikana maeneo mengi kwa kiwango kikubwa, hutumika kama dawa kwa kuku na mifugo mingine pia hutumika kama chakula kwa wanyama tofauti tofauti. Mmea huu una vitamin A na C.

### **Matumizi**

- Tumia majani kwa ujazo wa viganja viwili
- Ponda ponda/ saga na changanya kwenye maji lita 10
- Chuja na kuwapa kuku baada ya masaa 12 tangu kuitengeneza
- Itakayo baki baada ya masaa 12 mwaga na andaa nyingine.
- Wape kuku kwa siku 3-5

### **Magonjwa inayo yatibu**

Homa ya matumbo

Kipindu pindu cha kuku

KIderi/mdondo

Mafua



## **Mmea wa mlonge**

### **2. Pilipili kichaa**

Ianike ka kuisaga au kuiponda ponda, weka vijiko viwili vya pilipili kwenye maji lita 10-20, wape kuku wanywe kwa muda wa siku 3, kuku wakinywa dawa watapiga chafya mfululizo nah ii ni kiashiria kwamba dawa inafanya kazi ipasavyo. Dawa hii husaidia kuponya mafua kwa kuku.

### **3. Shubiri mwitu/ Aloe vera**

Huu ni mmea ambao huota porini na upatikanaji wake si mgumu kwa maeneo mengi, maandalizi ya dawa yanategemea umri wa kuku

- Tumia majani 3 ya shubiri mwitu yakate kate na kuyaloweka kwenye maji lita 10 kwa masaa 12
- Tumia maji ya dawa kwa kuku kwa muda wa siku 5 -7
- Bdilisha maji ya dawa kila baada ya masaa 12 **Magonjwa**

#### **yanayotibika**

- Homa ya matumbo ( Typhoid)
- Mafua( Corryza)

- Kipindupindu cha kuku( Fowl cholera)
- Kideri/mdondo



**Shubiri mwitu**

#### **4. Ndulele/Ndula, Tumgurusi, Makonde**

Majani hutibu minyoo na matunda hutibui vidonda kwa kuku



**Mmea wa ndula**

## 5. Mpapai

Wakatie Katie na kuyaloweka kisha wawekee kuku kwenye maji lita 6, majani ya papai hutibu minyoo, na homa ya matumbo.



**Jani la mpapai**

## 6. Mbarika (Nyonyo)

Hii hutibu uvimbe Kwa kuku, weka majani ya mbarika ndani ya jani la mgomba kisha weka kwenu\ye jivu la moto na ukande sehemu yenya uvimbe kwa kutumia majani ya mbarika.



**Mmea wa mbarika**

## 7. Mtakalang'onyo( Euphorbia Hirta)

Tumia majani ma tano ponda ponda na loweka kwa masaa 12, wape kuku kwa masaa 12 kisha badilisha dawa.

### Magonjwa inayo tibu

- Kideri/Mdondo wape kabla ya kuchanja
- Gumboro
- Ndui
- Kuhara damu/ Coccidiosis



**Mmea wa mtakalang'onyo**

## 8. Minyaa/ Cactus

Mmea huu huota maeneo mengi yenye asili ya ukame, ni mmea wenye uwezo wa kutunza maji kwa muda mrefu na ina miiba, Tumia tawi moja la mmea huu ponda ponda na kuchanganya kwenye maji lita 10-20 na kuwapa kuku kwa masaa 12.

### Magonjwa yanayotibika

- Vidonda



- Ngozi
- Uzazi

### **Faida ya kutibu kuku Kwa dawa za asili**

- i. Hupatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu
- ii. Hutibu magonjwa mengi
- iii. Hazina madhara kwa mlaji wa nyama au mayai



**Mnyaa/Cactus**

## **TUNAUZA VIFAA AINA VYOTE VYA UFUGAJI WA KUKU KAMA VILE;**

- 1** Cages za kisasa za kuku wa mayai na nyama.|kuku wa kubwa na vifaranga|
- 2** Mashine za kisasa za kutotoleshea vifaranga|full automatic incubator|kuanzia mayai 16 hadi 15000.
- 3** Taa za joto maalumu za kulelea vifaranga|Infrared| 4 heater za feni za kulelea vifaranga.
- 5** vifaa vyote vya kuundia mashine|incubator accessories|
- 6** Nipple za kunyweshea maji Kuku.
- 7** Mzani wa digital wa kupima chakula cha kuku|kg 50|kg300|
- 8** Tunafunga mifumo yote ya kunyweshea maji kuku na chakula.
- 9** Tunajenga mabanda ya kisasa ya ufugaji kuku.
- 10** Tunauza vifaranga wa kuku wa kienyeji na kisasa|siku|mwezi|
- 11** Tunauza mayai yenye sifa ya kutotoleshea vifaranga.
- 12** Tunauza mashine ya yakutengeneza chakula chenga chenga cha kuku|manual|automatic|
- 13** Tunauza hydroponics fodder tray.
- 14** Tunauza tochi maalumu ya kupimia yai lenye mbevu.

- 15** Tunauza digatal hygrometer|kipima joto bandani na incubator|  
16 Tunauza grinder and mixer machine.  
17 Tunauza mashine ya kukatia kuku midomo|manual|automatic|

**MAWASILIANO**

**0656446991**

**0747 608 608**

**DAR ES SALAAM -TEGETA NA GOBA**

**MWISHO**

